SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO

BALOZI MOHAMED RAMIA ABDIWAWA (MBM)

KUHUSU MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.

YALIYOMO

I.UTANGULIZI 1
II.MWENENDO WA UCHUMI.....5
III.UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA JULAI 2019 – MACHI 2020 17
A.Makadirio ya Mapato 17
B.Utekelezaji Halisi wa Mapato ya Serikali 19
C.Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi 20
IV.UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 22
V.UTEKELEZAJI HALISI WA MATUMIZI YA SERIKALI JULAI 2019 HADI MACHI 2020 30
i.Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu 31
ii.Matumizi ya Mfuko wa Miundombinu 32
VI.MATARAJIO YA MAPATO KWA MWAKA 2019/2020 33
A.Matarajio ya Mapato ya Ndani Julai – Juni 2019/2020 33
B.Matarajio ya Matumizi Julai 2019-Juni 2020 35
VII.MRIPUKO WA MARADHI YA COVID-19 NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA 37
VIII.MWELEKEO WA BAJETI 2020/2021- 2022/2023 46
Makadirio ya Mapato 48
Makadirio ya Ukusanyaji Kitaasisi.....48
Ruzuku na Mikopo kutoka Nje 49

Mwelekeo wa Matumizi 49
IX.MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO 52
X.SURA YA BAJETI 74
XI.MAENEO MAALUM.....78
XII.SHUKURANI 81
XIII.HITIMISHO: 86

HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO BALOZI MOHAMED RAMIA ABDIWAWA (MBM)

KUHUSU MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.

I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuendelea kuturuzuku neema zake kubwa na ndogo ikiwemo uhai, uzima na utulivu wa nchi yetu na ustawi wa watu wake uliotuwezesha kukutana kwa ajili ya kuzungumzia mambo yenye maslahi kwa maendeleo ya nchi yetu na watu wake.

2. **Mheshimiwa Spika,** Katiba yetu ya mwaka 1984 na Sheria ya Fedha za Umma ya namba 12 ya mwaka 2016 zinatoa wajibu kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha kutayarisha na kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka unaofuata wa fedha. Nakushukuru sana kwa fursa hii uliyonipa inayoniwezesha kutimiza wajibu huo ulio chini ya Kifungu cha 105 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu cha 41(3) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2016. Uwasilishaji wangu huu pia utapelekea Baraza lako tukufu nalo kutimiza wajibu wake wa

kujadili na hatimae kuidhinisha mapendekezo hayo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2020/2021.

3. **Mheshimiwa Spika,** leo ni mwezi wa sita (Juni) wa mwaka 2020; takriban miaka kumi tokea Novemba 2010 ambapo Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein alipata, kwa mara ya kwanza, imani na ridhaa ya Wazanzibari ya kuwa mkuu wa nchi yao ya Zanzibar, Rais na pia Mwenyekiti wa Baraza letu tukufu la Mapinduzi. Aidha, hiki ni kipindi chake cha pili tokea mwaka 2016 baada ya kuchaguliwa na wananchi kufuatia ridhaa ya Chama kilichoongoza nchi hii kwa zaidi ya miaka 40 sasa, Chama Cha Mapinduzi. Ukichanganya na kipindi kilichoongozwa na mojawapo ya Chama kiasisi kwa CCM, Chama cha Afro Shirazi, cha kuanzia tarehe 12 Januari 1964, vyama hivi vya Ukombozi na Mapinduzi vimeshaongoza nchi yetu kwa uweledi na mafanikio makubwa kwa miaka 56 sasa.

4. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt Ali Mohamed Shein, Mwanamapinduzi wa saba kuiongoza Zanzibar, kwa uongozi wake mahiri, wa hekima, uvumilivu wa mfano na uadilifu mkubwa ulioimarisha sana umoja wetu Wazanzibari wapenda amani, uliodumisha Mapinduzi yetu na uliopelekea maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii nchini petu, nitayoyagusia kwa mukhtasari baadae kidogo.

5. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya awamu hii ya saba ya Serikali yetu ya Mapinduzi yana mchango mkubwa wa msaidizi wa karibu wa Mheshimiwa Dkt. Shein, Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi. Kwa umoja wao, hii ***ni timu ya ushindi; timu ya umoja na timu ya maendeleo.*** Hongera sana Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Dkt. Shein, na bila ya kusita wala kuchoka. Kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kidemokrasia ya kuchagua uongozi wa nchi yetu, tukijaaliwa baadae mwaka huu tutakuwa na Uchaguzi Mkuu utaoweka uongozi mpya. Hivyo leo hii nawasilisha mapendekezo ya mwisho ya Bajeti ya Serikali kwa awamu hii ya saba ya SMZ. Kwangu ni fahari na bahati kubwa kuwasilisha Bajeti hii.

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa mfumo wa uongozi wa nchi yetu unaotokana na Muungano wetu wa Jamhuri mbili huru zilizounda Jamhuri moja ya Muungano wa Tanzania, tokea mwezi April 1964 Zanzibar imekuwa sehemu ya Jamhuri hiyo ya Muungano. Kwa sababu hiyo, utulivu wa Zanzibar, usalama na maendeleo yake unategemea sana uhusiano wake na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Tunajivunia uhusiano mzuri ambao umekuwepo na unaimarika muda wote. Kwa kipindi hiki, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wake Mhe. Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa.

Tunawashukuru sana kwa uongozi wao, nia yao ya dhati ya kuiletea maendeleo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mashirikiano mazuri na SMZ.

7. **Mheshimiwa Spika,** chini ya mfumo wetu wa uendeshaji wa nchi, dola inaongozwa na mihimili mitatu ambapo kila mmoja ukiwa unajitegemea na uhuru katika usimamizi wake. Zaidi ya mhimili wa Serikali, dola lina pia Mhimili wa Baraza la kutunga Sheria (la Wawakilishi) ambalo kwa miaka mitano inayomalizika, limeongozwa kwa uweledi mkubwa na wewe Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, katika nafasi yako ya Spika wa Baraza hili la Wawakilishi wa Wazanzibari wote. Mhimili wa tatu ni wa Mahakama, ambao upo maalum kwa ajili ya kusimamia upatikanaji wa haki kwa watu wote, kwa mujibu wa Sheria tulizojitungia. Mhimili huu kwa kipindi hiki nao umeongozwa kwa ustadi mkubwa na Mheshimiwa Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar. Kwa dhati kabisa, naomba nikupongezeni sana Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid na Mheshimiwa Jaji Omar Othman Makungu kwa uongozi wenu uliopelekea kuwepo kwa maelewano makubwa baina ya mihimili hiyo mitatu ya Dola, bila ya kuathiri uhuru na utendaji wake. Hongereni sana. Sisi sote tumekuwa na imani nanyi wakati wote.

8. **Mheshimiwa Spika,** kwa sababu maalum nilizozitaja za kumalizika kwa kipindi cha pili cha awamu hii ya

saba ya SMZ, naomba uniruhusu kuwasilisha kwa mukhtasari tu, mafanikio ya utendaji wa awamu hii ya Serikali kwani haiwezekani kuyataja yote kikamilifu. Kwa ufupi kwa kipindi chote hiki cha miaka 10, ilani ya CCM imetekelezwa kwa zaidi ya asilimia 95.

II. MWENENDO WA UCHUMI

9. Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa maendeleo ya nchi yanatokana na mafanikio yake katika kukuza na kuleta mageuzi ya uchumi wake na ya watu wake. Aidha mafanikio yaliopatikana yametokana na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha 2010 – 2015 na 2015 – 2020. Ilani hiyo imeweka dira imara ambapo Dkt. Ali Mohamed Shein amekuwa kinara wa kusimamia pamoja utekelezaji wa mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini (MKUZA) uliokwenda sambamba na utekelezaji wa malengo ya Jumuiya ya MDGs na kimataifa ya SDGs. Miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyosajiliwa Zanzibar kuanzia mwaka 2010 ni haya yafuatayo:-

i. *Kuongezeka Pato halisi la Taifa* kutoka thamani ya TZS 1.768 trilioni mwaka 2010 hadi TZS 3.078 trilioni mwaka 2019. Kwa wastani, uchumi umekuwa kwa asilimia 6.1 kwa mwaka katika kipindi hicho. Kutokana na ukuaji huo, wastani wa Pato la mtu binafsi nao umeongezeka kutoka

Shilingi 942,000 sawa na Dola 675 mwaka 2010 hadi Shilingi 2,549,000 sawa na Dola 1,114 mwaka 2019;

ii. Kuwepo kwa *utulivu wa bei* ambapo katika kipindi chote hicho kiwango cha mfumko wa bei kilikuwa cha tarakimu moja na muda mwingi chini ya asilimia 5;

iii. Kuwepo kwa *utulivu wa Shilingi ya Tanzania* dhidi ya fedha za kibiashara hususan Dola ya Kimarekani;

iv. *Kuimarika kwa uwekezaji mitaji* nchini na hivyo utanuzi wa ajira ambapo mitaji iliyoidhinishwa imeongezeka kutoka Dola za Kimarekani 15.2 milioni mwaka 2010 hadi kufikia Dola za Kimarekani 393.7 milioni mwaka 2019. Aidha, idadi ya ajira katika miradi hiyo imeongezeka kutoka ajira 2,307 mwaka 2010 hadi ajira 4,859 mwaka 2019;

v. *Kuongezeka kwa ajira:* Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka kumi jumla ya watu 30,649 waliajiriwa wakiwemo 11,823 walioajiriwa na Serikali na taasisi zake na 18,826 walioajiriwa na sekta binafsi. Sambamba na ajira hizo, Serikali pia ilisaidia watu kujiajiri wenyewe kwa kuwapatia mtaji kupitia mfuko wa Uwezeshaji na Programu ya ajira kwa Vijana kwa Mkopo nafuu;

vi. *Kuzidi kupungua hali ya umaskini nchini* ambapo taarifa za awali za matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2019 zinaonesha kuwa kwa ujumla, idadi ya watu wanaoishi katika umaskini wa mahitaji ya lazima (basic needs poverty) imepungua kutoka asilimia 30.4 mwaka 2014 hadi asilimia 25.7 mwaka 2019 wakati wanaoishi katika umaskini wa chakula (food poverty) wamepungua kutoka asilimia 10.8. hadi 9.3 katika kipindi hicho;

vii. *Kuimarika kwa mapato ya ndani* ya Serikali kutoka TZS 221.7 bilioni mwaka 2010/2011 hadi TZS 741.2 bilioni mwaka 2018/2019. Mafanikio hayo yalikwenda sambamba na kuimarika kwa kujitegemea kufuatia kupungua sana utegemezi wa Bajeti kutoka asilimia 30.2 mwaka 2010/2011 hadi asilimia 5.1 mwaka 2018/2019 kwani awamu ya saba imeongeza Bajeti yake kwa mara 3.2 kutoka shs. 444.6 bilioni mwaka 2010/2011 hadi TZS. 1.4 trilioni mwaka 2019/2020.

10. Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ya kiuchumi yanabainika katika Sekta za uzalishaji yakiwemo yafuatayo:

i. Kilimo:

11. Mheshimiwa Spika, kila mwananchi ameshuhudia kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na

biashara katika kipindi cha miaka 10 hii ambapo uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka TZS 130.3 bilioni mwaka 2010 hadi TZS 309.5 bilioni mwaka 2019. Mafanikio makubwa yamepatikana katika zao adhimu la Karafuu ambapo mwaka 2011 Serikali ilifanya mapitio ya mfumo mzima wa Biashara ya Karafuu na Sheria No. 11 ya 2011 ya Shirika la Biashara la Taifa iliundwa.

12. Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 umejitokeza kuwa na mavuno makubwa zaidi kuwahi kurekodiwa katika kipindi cha zaidi ya miaka 30 iliyopita. Mafanikio haya yanatokana na uamuzi maalum wa Serikali chini ya uongozi wa Dkt. Shein wa kutobinafsisha zao hili na kuwapatia wakulima wa Karafuu bei nzuri kwa mauzo yao. Wakati Serikali imeamua kuwapatia wakulima hao asilimia 80 ya bei ya soko la kimataifa, Dkt. Shein alihakikisha kuwa bei ya kununulia Karafuu kutoka kwa mkulima haishuki TZS 14,000 kwa kilo kwa kipindi chote cha miaka 10 iliyopita. Kabla ya bei hii, kilo moja ya Karafuu ilinunuliwa kwa wastani wa shs. 5000 tu. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 180 kwa kilo.

ii. Viwanda:

13. Mheshimiwa Spika, mafanikio katika uwekezaji viwandani ni madogo kulinganisha na sekta nyengine za kiuchumi na nidhahiri kuwa jitihada zaidi zinahitajika za kuvutia uwekezaji katika sekta hii muhimu kwa

maendeleo. Hata hivyo, bado mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi hichi ambapo uwekezaji viwandani umeendelea kukua na hivyo kuongeza mchango wa Sekta hii katika Pato la Taifa kutoka asilimia 17.1 mwaka 2010 hadi asilimia 18.3 mwaka 2019.

iii. Huduma:

14. Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi wa Dkt. Shein, sio tu kwamba Sekta ya huduma imeendelea kuongoza katika kuchangia Pato la Taifa, sekta hiyo imeimarika zaidi. Mafanikio hayo yanajidhihirisha katika kuimarika kwa huduma za Utalii ambapo idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar imeongezeka mara nne kutoka watalii 132,836 mwaka 2010 hadi watalii 538,264 mwaka 2019. Aidha, katika kipindi hicho, huduma za kifedha katika benki za biashara zimeimarika kama inavyodhihirishwa na kuongezeka kwa rasilimali Mabenki kutoka TZS 321.5 bilioni mwaka 2010 hadi TZS 988.4 bilioni mwaka 2019. Matawi yapatayo 13 kutoka nje ya Zanzibar na taasisi nyengine za fedha na Bima zikatoa huduma zao hapa zanzibar.

iv. Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia:

15. Mheshimiwa Spika, uimara wa uongozi wa Dkt. Shein umejidhihirisha pia katika kushirikiana kwake na viongozi wakuu wa Serikali ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania na kuyapatia ufumbuzi mambo yaliyoonekana kuwa magumu, likiwemo suala la usimamizi wa Mafuta na Gesi Asilia. Kupitia kwake na Rais Mstaafu wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

16. **Mheshimiwa Spika,** Wazanzibari wote wakweli na wapenda maendeleo wana deni la shukurani kwa Dkt. Kikwete na Dkt. Shein kwa makubaliano yao yaliyopelekea Zanzibar kusimamia yenyewe rasilimali hiyo ya Mafuta na Gesi. Kufuatia mabadiliko hayo, Sera, Sheria na Mkataba wa mfano wa ugawanaji wa mafuta na gesi viliandaliwa na kuidhinishwa. Aidha, Mkataba wa mwanzo wa utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi asilia umesainiwa katika kipindi hichi hapo Oktoba 2018. Wakati tukielewa kuwa hakuna ugunduzi wa rasilimali hiyo muhimu hadi sasa, sisi wananchi wa Zanzibar bado tunapongeza sana mafanikio haya ya uongozi wa Dkt. Shein.

MAENDELEO NA HUDUMA ZA JAMII

17. **Mheshimiwa Spika,** ili ukuaji wa uchumi uwe wa manufaa kwa nchi, unapaswa uendane na maendeleo ya wananchi yanayoonekana katika hali zao za maisha na upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii kama vile elimu, afya, maji safi na salama na mazingira ya kuishi kwa ujumla. Kwa hili, Dkt. Shein anastahili pongezi nyengine maalum kwa mafanikio makubwa katika

kipindi cha uongozi wake. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:

v. Elimu:

18. Mheshimiwa Spika, kufuta ujinga wa kusoma na kuandika imejitokeza kuwa na msisitizo maalum kwa SMZ, kutokana na historia yake ambapo watoto wa kinyonge walinyimwa fursa ya kupata elimu iliyo bora. Miaka 10 ya awamu ya saba ya SMZ chini ya mwanamapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein imeendeleza kwa kasi kubwa upatikanaji wa elimu kwa watoto wote katika kila kona ya nchi yetu, mijini na mashamba, Pemba na Unguja. Mifano ya mafanikio hayo ni kuongezeka kwa Bajeti ya Elimu kutoka TZS 47.093 bilioni mwaka 2010/2011 hadi TZS 178.917 bilioni mwaka 2019/2020; kuimarika upatikananji wa elimu kwa watoto wa kike kunakodhihirishwa na usawa wa usajili wa wanafunzi katika ngazi zote za masomo kutoka maandalizi hadi vyuo vikuu; kuimarika kwa mazingira ya kusomea watoto wetu kwa kujengwa madarasa ya kutosha katika kipindi hicho na kupatiwa samani na vitabu vya rejea na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi katika ngazi zote.

vi. Afya:

19. Mheshimiwa Spika, kati ya mafanikio makubwa katika miaka hii 10 ya uongozi wa Dkt. Shein ni kuimarika kwa huduma za afya. Uimarikaji huo umefanyika katika

mfumo wa utoaji wa huduma kwa kuweka bayana ngazi tofauti za huduma kutokea za msingi hadi rufaa; kuimarika kwa miundombinu na vifaa vya kutolea huduma hizo, ikiwemo kuanza ujenzi wa hospitali mpya ya rufaa na kufundishia hapo kwenye eneo la mita za mraba 579,864.9 hapo Binguni, matengenezo makubwa ya hospitali ya Mnazimmoja. Mwembeladu na Kidongochekundu. Aidha, hospitali za Abdalla Mzee (Mkoani), Kivunge na Makunduchi zimepandishwa hadhi na kufanyiwa matengezo makubwa wakati maandalizi kwa matengenezo makubwa ya hospitali ya Wete nayo yakifikia hatua kubwa baada ya kupatikana kwa ufadhili kutoka Falme za Kiarabu.

20. Mheshimiwa Spika, sambamba na mafanikio haya, Serikali pia imetanua huduma za afya kwa kuanza kutoa huduma za usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo na tiba kwa wagonjwa wa saratani. Aidha, kazi kubwa imefanyika katika kuimarisha upatikanaji wa dawa ambapo Serikali imeongeza bajeti ya kununulia dawa kutoka TZS 500 milioni mwaka 2010/2011 hadi TZS 17 bilioni mwaka 2020/2021. Huduma za afya sasa zipo kila mahala mijini na vijijini si kwa zaidi ya masafa ya kilomita tano.

21. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho mafanikio makubwa yamepatikana kwa kuongeza idadi ya madaktari wazalendo kutoka 25 mwaka 2010 hadi kufikia 304 mwaka 2019. Kati ya hao, madaktari

bingwa wameongezeka kutoka watatu mwaka 2010 hadi madaktari bingwa 57 mwaka 2019. Kutokana na mafanikio hayo, kwa sasa daktari mmoja anatibu wastani wa wagonjwa 6,276 ikilinganishwa na wastani wa wagonjwa 31,838 mwaka 2010.

vii. Maji Safi na Salama:

22. Mheshimiwa Spika, vitabu vitakatifu vimetufunza kuwa "hakuna uhai pasipo na maji". Katika miaka 10 ya awamu ya saba ya SMZ upatikanaji wa maji safi na salama umeimarika sana, Unguja na Pemba, mjini na mashamba. Kwa wastani, upatikanaji wa maji umeongezeka kutoka asilimia 80 mwaka 2010 hadi asilimia 90 mwaka 2019 kwa maeneo ya mjini na kutoka asilimia 60 hadi 80 kwa maeneo ya mashamba.

viii. Mazingira ya Kuishi:

23. Mheshimiwa Spika, Utu wa binaadam unahitaji kuwa aishi katika maeneo yenye staha na hadhi ya kuishi watu. Moja ya mambo yaliyowekewa mkazo baada ya Mapinduzi ni mazingira bora ya kuishi ambapo SMZ ilijenga nyumba bora na za kisasa katika maeneo mbalimbali ya miji na baadhi ya mashamba na kuwagawia wananchi. Kwa bahati mbaya, hali ya uchumi wa nchi haikuruhusu kuendelezwa kwa jambo hilo muhimu kwa kipindi kirefu.

24. Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika miaka 10 hii, Serikali imeanza tena kuimarisha makaazi ya watu ikiwemo katika maeneo ya Mbweni, kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, mji mpya wa Kwahani, kijiji cha Dundua kwa wananchi walioathirika na kutengwa kwa eneo la bandari ya Mafuta na Gesi Mangapwani na Nungwi kwa wananchi waliokuwa wanaathiriwa na maji ya mvua. Ujenzi wa Ofisi za Serikali nao unaendelea vizuri. Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Katiba na Sheria hapo Mazizini, jengo la Ofisi za Serikali, Gombani, jengo la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA), jengo la Mtakwimu Mkuu wa Serikali ni baadhi ya mifano ya mafanikio hayo;

25. Mheshimiwa Spika, Kwa mnasaba huo wa kuimarisha mazingira ya kuishi, maeneo mengi ya mji wa Zanzibar na miji ya Wete, Chake-Chake na Mkoani kwa Pemba yamewekwa taa za barabarani, huduma za usafi wa jiji la Zanzibar zimeimarishwa na, kubwa zaidi, tatizo la kutuwama kwa maji ya mvua katika maeneo mengi ya jiji la Zanzibar, Mwanakwerekwe, Kiembesamaki na Kibonde Mzungu limepatiwa ufumbuzi, ikiwemo kwa ujenzi wa zaidi ya kilomita 22 za misingi ya maji ya mvua na wa daraja la Dkt. Ali Mohamed Shein hapo Kibondemzungu.

ix. Maeneo mengine ya mafanikio makubwa:

a. Usafiri na Usafirishaji – Serikali imenunua meli mpya za abiria na mafuta ili kutoa huduma za usafiri kwa wananchi (M.V. Mapinduzi II) na usafirishaji wa mafuta (M.T Ukombozi II) na kufanikisha uwekezaji zaidi wa Sekta binafsi katika usafiri wa kisasa;

b. Meli hizo zimeigharimu SMZ zaidi ya TZS. bilioni mia moja. Kuimarishwa kwa Taasisi za Umma za Bandari, Umeme (ZECO), Maji (ZAWA) na kadhalika.

c. Kuimarishwa kwa Vyombo vya Habari ikiwemo Shirika la Utangazaji (ZBC) ambalo limepatiwa mitambo mipya na ya kisasa na Shirika la Magazeti; na

d. Kuimarika kwa maslahi ya watumishi wa umma kwa kuongeza mishahara ya kima cha chini katika vipindi vinne tofauti kutoka TZS. 80,000 mwaka 2010 hadi TZS 300,000 kwa mwezi hivi sasa sambamba na kuimarisha maslahi ya wataalamu.

26. Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na haya yafuatayo:

e. Kuimarika kwa Utumishi wa Umma na maslahi ambapo mishahara ya wafanyakazi imefanyiwa

marekebisho mara nne. Pencheni ya wastaafu nayo imeimarishwa ikiwemo kwa viongozi wastaafu; na

f. Kuimarisha michezo nchini kwa kujenga viwanja katika Wilaya 5 hivi sasa

g. Kuimarishwa kwa huduma za makundi yenye mahitaji maalum na kutolewa kwa pencheni ya jamii kila mwezi kwa wazee wote wenye umri wa miaka 70 na zaidi. Mwaka 2016 wazee hao wapatao 21,000 walifaidika na sasa idadi ya wazee 28,000 wanapata pencheni ya jamii.

x. Mafanikio mengine muhimu chini ya uongozi wa Dkt. Shein ni kuimarika kwa utawala bora ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:

a) Kuimarika kwa Demokrasia ikiwemo kushirikiana na vyama vingine vya siasa katika kuendesha Serikali.

b) Kuimarika usimamizi wa maadili ya viongozi na watendaji wa umma ikiwemo kwa kuanzishwa Tume maalum ya kusimamia maadili;

c) Kuimarika kwa uhusiano wa Serikali na BLW ambapo jumla ya miswada 120 ya Sheria iliwasilishwa na kupitishwa na Baraza hili la tisa hadi leo; na

d) Kuimarika kwa uhusiano na Mahkama na ujenzi wa Mahkama Kuu mpya hapo Tunguu.

27. Mheshimiwa Spika, hii ni sehemu ndogo sana ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 hii. Kwa sababu ya muda, haitoyumkinika kuyataja yote hapa lakini nna hakika Waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako watayataja na mengi mengine katika michango yao kwenye hotuba hii. Kwa sasa naomba tu uniruhusu niendelee na kuwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2019/2020.

III. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA JULAI 2019 – MACHI 2020

A. Makadirio ya Mapato

28. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Baraza lako tukufu liliidhinisha makadirio ya Serikali ya kukusanya jumla ya TZS 1.419 trilioni ikijumuisha maeneo yafuatayo:

i. Mapato kutoka vianzio vya ndani Jumla ya TZS 976.5 bilioni;

ii. Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo Jumla ya TZS 394.6 bilioni, ikiwemo mikopo ya TZS 299.1 bilioni na ruzuku TZS 95.5 bilioni;

iii. Ruzuku ya Mfuko wa Pamoja na wa Washirika wa Maendeleo (Basket Fund) TZS 8.3 bilioni; na

iv. Mikopo ya ndani ya TZS 40 bilioni.

29. Mheshimiwa Spika, kati ya mapato ya ndani ya TZS 976.5 bilioni, jumla ya TZS 859.7 bilioni zilitarajiwa kutokana na makusanyo ya vyanzo vya kodi na TZS 116.8 bilioni ni kutokana na vyanzo visivyo vya kodi kwa mgawanyo ufuatao:

i. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) TZS 488.5 bilioni sawa na asilimia 50 ya makadirio ya mapato ya ndani;
ii. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) TZS 350.2 bilioni sawa na asilimia 36 ya makadirio ya mapato ya ndani;
iii. Mapato ya Mawizara TZS 99.3 bilioni sawa na asilimia 10 ya makadrio ya mapato ya ndani;
iv. Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT TZS 21.0 bilioni sawa na asilimia 2 ya makadirio ya mapato ya ndani;
v. Gawio la faida kutoka Benki Kuu (BoT) TZS 9.5 bilioni sawa na asilimia 1 ya makadirio ya mapato ya ndani; na
vi. Gawio la faida kutoka katika Mashirika ya SMZ TZS 8.0 bilioni sawa na asilimia 0.8 ya makadirio ya mapato ya ndani.

B. Utekelezaji Halisi wa Mapato ya Serikali

30. Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2019 – Machi 2020) Serikali imekusanya jumla ya TZS 807.7 bilioni sawa na asilimia 74 ya lengo la TZS 1,085.3 bilioni zikiwemo mapato ya ndani ya TZS 648.2 bilioni sawa na asilimia 85.8 ya makisio ya TZS 755.5 bilioni kwa kipindi hicho na mapato kutoka vianzio vyengine ni TZS 160.9 bilioni kwa mchanganuo ufuatao:

i. Mapato kutoka nje ni TZS 127.7 bilioni sawa na asilimia 43 ya makisio ya TZS 296 bilioni. Kati ya kiasi hicho, Ruzuku ni TZS 33 bilioni na Mikopo ni TZS 94.7 bilioni;
ii. Mikopo ya ndani TZS 26.3 bilioni sawa na asilimia 82 ya makisio ya TZS 32 bilioni;
iii. Fedha kutoka Mfuko wa Pamoja na Washirika wa Maendeleo ni TZS 2.8 bilioni; na
iv. Misaada ya Kibajeti (GBS) TZS 4.1 bilioni.

31. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mapitio mapato ya ndani ya TZS 648.2 bilioni yanamaanisha ukuaji wa asilimia 11.9 ikilinganishwa na TZS 579.3 bilioni zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Kati ya makusanyo hayo, mapato ya kodi yamefikia TZS 555.4 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 83.8 ya makadirio, na hivyo kuashiria ukuaji wa asilimia 8.3. Mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia TZS 92.8 bilioni, takriban sawa lengo la kipindi hicho

na kufikia utendaji wa asilimia 100.5 ya makadirio. Kiasi hicho kinamaanisha ukuaji wa asilimia 39.1 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 66.7 bilioni yaliyopatikana kipindi kama hicho mwaka uliopita. Ukuaji huo umechangiwa zaidi na malipo ya TZS 25.78 bilioni yaliyolipwa na Kampuni ya Zantel kwa matumizi ya Mkonga wa Taifa na gawio kutoka mashirika ya SMZ la jumla ya TZS 4.9 bilioni.

C. Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi

i. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)

32. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, ZRB ilikusanya jumla ya TZS 316.8 bilioni sawa na asilimia 81.7 ya makadirio ya TZS 387.9 bilioni. Mapato hayo yanaonekana kuongezeka kwa asilimia 12.7 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 281.2 bilioni kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/2019.

ii. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) – Zanzibar

33. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mapitio TRA imekusanya jumla ya TZS 222.9 bilioni na hivyo kufikia asilimia 85.9 ya makadirio ya TZS 259.5 bilioni na pia yakionesha ukuaji wa asilimia 2.5 kutoka makusanyo ya TZS 217.4 bilioni zilizokusanywa katika miezi tisa ya

kwanza ya mwaka uliopita wa fedha. Kati ya mapato hayo, Idara ya Forodha imekusanya jumla ya TZS 117.5 bilioni sawa na asilimia 88.3 ya makadirio ya kipindi hicho ya TZS 133.2 bilioni na Idara ya Kodi za Ndani imekusanya jumla ya TZS 105.4 bilioni sawa na asilimia 83.4 ya lengo la kukusanya TZS 126.3 bilioni. Mapato kutokana na kodi za Forodha yameathiriwa na changamoto za uingiaji wa bidhaa kutokana na tatizo la Bandari ya Malindi.

iii. Kodi ya Mapato kwa Wafanyakazi wa SMT

34. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya TZS 15.7 bilioni zimeweza kukusanywa kutokana na wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar ambazo ni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho.

iv. Mapato ya Mfuko wa Miundombinu

35. Mheshimiwa Spika, Jumla ya TZS 26.5 bilioni zimekusanywa kupitia Mfuko wa Miundombinu kwa kipindi cha miezi tisa, sawa na asilimia 85.2 ya makadirio ya TZS 31.1 bilioni. Kati ya kiasi hicho, ZRB imekusanya TZS 17.9 bilioni sawa na asilimia 90.0 ya makadirio ya TZS 19.9 bilioni na TRA imekusanya jumla ya TZS 8.6 bilioni sawa na asilimia 76.6 ya lengo la kukusanya TZS 11.2 bilioni.

IV. UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

36. Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2019, Baraza la Wawakilishi liliidhinisha marekebisho katika Sheria mbalimbali kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa Mapato ya Serikali. Matokeo ya utekelezaji wa baadhi ya hatua hizo ni kama ifuatavyo:

Hatua Zinazohusiana na Mabadiliko ya Sheria

i. Kufanya Mabadiliko ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya Mwaka 1998

37. Mheshimiwa Spika, Serikali iliidhinisha kufuta sharti la ziada la kiwango cha Dola 100 kwa mgeni kwa siku ikiwa ni miongoni mwa kigezo cha Hoteli kusajiliwa katika mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ili kuondoa changamoto mbalimbali zilizojitokeza. Marekebisho ya Kanuni ya Kodi ya Ongezeko la Thamani za mwaka 2012 yamefanyika katika kifungu cha 4(2) kwa kuondosha kigezo hicho cha ziada. Hadi kufikia Machi 2020 Hoteli mbili zimewasilisha maombi na kusajiliwa katika mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kuondoshwa katika Ushuru wa Hoteli.

ii. Kufanya Mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli Nam. 1 ya mwaka 1995

38. Mheshimiwa Spika, hatua hii ilikuwa na lengo la kuwaingiza katika wigo wa kodi pamoja na kuwatoza kodi wageni wote wanaolala katika vyombo vya baharini ili kuweka usawa katika mfumo wa kodi na kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali. Sheria ya Hoteli Namba. 1 ya mwaka 1995 imerekebishwa kwa kuingiza maana ya neno "Meli ya Kitalii" na kifungu cha 3(2) kimerekebishwa kwa kuingiza maneno "Meli ya Kitalii" ili kuzifanya meli za kitalii kuwa na sifa ya kutozwa kodi. Aidha, Jadweli la Sheria ya Hoteli limerekebishwa kwa kuingiza kipengele cha 4 kwa kuweka kiwango cha dola 8 kwa mgeni kwa siku atayelala katika "Meli ya Kitalii". Utekelezaji wa hatua hii umeanza Julai, 2019 na hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya vyombo 3 vyenye Idadi ya abiria 990 viliingia nchini na jumla ya USD 9,734 zimekusanywa.

iii. Mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam.7 ya mwaka 2017

39. Mheshimiwa Spika, Mkakati wa hatua hii ulikuwa na lengo la kuzitambua na kuzisajili gari zenye uwezo wa kubeba mizigo chini ya tani moja zinazojishughulisha na biashara na kuziingiza gari hizo katika wigo wa kodi na kulinda mapato ya Serikali. Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 7 ya mwaka 2017 imerekebishwa katika

Jadweli la Tatu kwa kuweka kipengele namba 8 kwa kuziingiza katika wigo wa kodi gari hizo.Utekezaji wa hatua hii umeanza Julai mwaka 2019 ambapo gari 1,095 zimesajiliwa na jumla ya TZS 109.5 milioni zimekusanywa hadi kufikia mwezi Machi, 2020.

Hatua za Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi

a. Kumarisha mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato katika Wizara na Taasisi za Serikali

40. Mheshimiwa Spika, Serikali ilidhamiria kuweka mfumo maalum wa malipo kupitia benki (Revenue Gateway) ili kuongeza ufanisi wa usimamizi na udhibiti wa mapato ya Serikali na kurahisisha malipo kwa njia tofauti ikiwemo mitandao ya simu, wakala wa Benki ya PBZ au kupitia benki ya PBZ moja kwa moja. Tayari Mfumo huo umewekwa kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar na Wizara imeanza kutumia huduma za ezypesa na "Mobile Banking" katika ulipaji wa ada na tozo na hutumia namba maalum (Control Number) kuweka udhibiti wa mapato. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2020, Serikali ilikusanya Jumla ya TZS 92.8 Bilioni ambazo ni ongezeko la asilimia 39.1 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 66.7 Bilioni kwa mwaka 2018/19.

b. Kuimarisha Usimamizi na Ufuatiliaji wa Mapato

41. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia ZRB na TRA ilipanga kuchukuwa hatua zifuatazo kwa lengo la kuhakikisha kwamba inaimarisha mifumo ya usimamizi wa mapato:

i. Kuoanisha mifumo iliyopo baina ya taasisi za ukusanyaji wa mapato na taasisi nyengine za Serikali ili kupata taarifa zaidi za walipakodi, ambapo hadi kufikia Machi 2020 kazi ya kuunganisha mifumo ya ZRB na wa Wakala wa Usajili wa Biashara (BPRA), mfumo wa malipo kati ya ZRB na PBZ, na ZRB na Benki Kuu imekamilika na kuanza kutumika. Mfumo wa Forodha (TANCIS) unaendelea kuimarishwa zaidi ili kuelekea kwenye mfumo mmoja utakaounganisha Taasisi nyengine za Serikali kwa kurahisisha taratibu za utoaji wa mizigo (Electronic Single Window).

ii. Kufanya uhakiki zaidi wa ritani na nyaraka mbalimbali zinazowasilishwa na walipa kodi kwa lengo la kubaini mianya ya ukwepaji wa kodi. Hatua hii imepelekea kukusanya jumla ya TZS 2.16 bilioni na USD 161,523.6 hadi kufikia Machi 2020. Aidha, Serikali imeunda timu maalum ya watendaji wakuu wa taasisi mbalimbali makhsusi kwa ajili ya kufuatilia ulipaji kodi kwa Mahoteli.

iii. Kufanya ukaguzi kwa walipa kodi ili kuhakikisha kodi sahihi ya Serikali inalipwa na hadi kufikia

Machi 2020 walipa kodi 71 wamefanyiwa ukaguzi na jumla ya TZS 2.57 bilioni na USD 410,304.29 zimegundulika kukwepwa na hivyo kudaiwa.

iv. Kusajili walipakodi 754 wapya na kurusha hewani vipindi 25 vya Redio na 6 vya Televisheni, kuandaa Semina 16 kwa walipakodi tofauti na kufanya mikutano 22 kwa lengo la kutoa elimu zaidi na kuongeza uwajibikaji.

c. Kugomboa madeni ya walipakodi

42. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2019/20, Serikali iliweka utaratibu maalumu wa kugomboa madeni ya kodi ambao ulihusisha kusamehe malimbikizo ya adhabu na riba kwa kiwango cha asilimia 100 kwa walipakodi wenye madeni waliopo ZRB. Hatua hii imepelekea kukusanya jumla ya TZS 638.25 milioni hadi kufikia mwezi wa Machi 2020.

d. Kuongeza muda na ufanisi wa Utoaji na Usafirishaji wa Mizigo kupitia Bandarini

43. Mheshimiwa Spika, Serikali katika kukabiliana na changomoto ya mrundikano wa mizigo katika bandari ya Zanzibar imeanzisha utaratibu wa kutoa huduma kwa saa ishirini na nne katika bandari hiyo. Kwa kiasi, hatua hii imeongeza ufanisi na kupunguza kidogo mrundikano wa makontena ambapo taratibu za usafirishaji mizigo zinakamilika ndani ya saa 6 na

taratibu za uingizaji mizigo zinakamilika ndani ya saa 30.

e. Kuwajengea uwezo watumiaji wa Mfumo wa Forodha (TANCIS)

44. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mapitio, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeendelea na hatua za kuwajengea uwezo mawakala wa Forodha na wafanyakazi wa Shirika la Bandari kwa utumiaji wa mfumo wa Forodha wa TANCIS. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yanayotokana na biashara ya Kimataifa, kupunguza gharama za kufanya biashara na kuchochea kasi ya mzunguko wa biashara. Hadi kufikia Machi 2020, mawakala wa Forodha 125, wafanyakazi wa Shirika la Bandari 20 na wafanyakazi 61 wa TRA waliopo Zanzibar wamepatiwa mafunzo hayo.

f. Kupunguza mianya ya kuepuka kodi (Tax avoidance)

45. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 TRA ilipanga kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Idara ya Kodi za Ndani katika nyanja za uhaulishaji wa bei (transfer pricing) na utozaji wa kodi ya mapato kwa kampuni zinazofanya biashara za kimataifa (International Taxation) kwa lengo la kukabiliana na udanganyifu wa njia za kisasa za kuepuka kulipa kodi. Hadi kufikia Machi 2020, wafanyakazi watano

wamepatiwa mafunzo hayo katika chuo cha Kodi (ITA) huko Dar-es-Salaam.

g. Mapitio ya Sheria na Kanuni zinazotoa Misamaha ya Kodi

46. Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga kufanya mapitio ya Kanuni za vigezo vya misamaha ya kodi ili ziweze kuendana na hali halisi ya mahitaji ya misamaha hiyo kwa sasa pamoja na kuziba mianya iliyojitokeza katika usimamizi na upotevu wa mapato ya Serikali. Utekelezaji wa kazi hii bado unaendelea na inategemewa kumalizika katika mwaka wa fedha ujao wa 2020/2021.

h. Ushajiishaji wananchi kudai risiti za kielektroniki

47. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali kupitia Bodi ya Mapato Zanzibar ilipanga kuandaa utaratibu wa utoaji wa risiti kwa mfumo wa kieletrokiki kwa lengo la kuondoa changamoto ya wafanyabiashara ya kutotoa risiti wakati wa mauzo. Hatua ya utengenezaji wa mfumo (software) imekamilika na majaribio ya mfumo yalianza rasmi mwezi Mei, 2020. Aidha, Mfumo wa usimamizi wa kodi kwa njia ya vitalu (block management system) umeanza kutumika katika maeneo ya majaribio kwa upande wa Unguja.

i. Mapitio ya Tozo Mbalimbali kwa Kuimarisha Mazingira ya Biashara

48. Mheshimiwa Spika, Eneo jengine lililoahidiwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni kufanya mapitio ya tozo na ada zinazotozwa katika sekta ya biashara, viwanda na huduma kwa lengo la kuimarisha mazingira ya biashara na kushajiisha ongezeko la usajili wa wafanyabiashara kuingia katika mfumo rasmi, hivyo kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato pamoja na ulipaji wa kodi, tozo na ada kwa hiari. Hatua hii ilikuwa na dhamira ya kupunguza au kufuta baadhi ya ada na tozo, kuondoa muingiliano wa utozaji wa ada na tozo na migongano ya majukumu ya kiutendaji baina ya Mamlaka za utoaji leseni, vibali na ruhusa nyengine na Mamlaka za Usimamizi.

49. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2020 Serikali imepitia na kuziainisha ada na tozo zote zinazosimamiwa na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa pamoja na kubainisha changamoto zinazohusiana na ada na tozo hizo. Mapitio ya tozo na ada za Sekta nane zinazohusiana na Uwekezaji, Utalii, Biashara, Viwanda, Uagiziaji na Usafirishaji wa Bidhaa, Kilimo (Mwani, Dagaa na Karafuu), Usafiri wa Baharini na Nchi kavu yamekamilika na zinachukuliwa hatua tofauti. Kazi ya kupitia ada na tozo zilizobakia na kufanya marekebisho mbali mbali ikiwemo kufuta au kupunguza ili kuondoa kero na urasimu kwa

wafanyabiashara na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa lengo la kuhamasisha kasi ya ukuaji wa uchumi katika sekta zilizobakia inaendelea.

j. Kuimarisha Usimamizi wa Ardhi

50. Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya utafiti uliofanyika juu ya ukodishwaji wa Ardhi, Serikali kupitia Tume ya Mipango na Kamisheni ya Ardhi kwa mwaka 2019/2020 ilipanga kupitia upya viwango vya ukodishaji wa Ardhi (Lease Rent) na mikataba yote iliyokwisha kutolewa ya ukodishaji wa visiwa au sehemu yake. Kazi hiyo tayari imekamilika na inategemewa kutumika rasmi Julai mwaka 2020 baada ya kusainiwa na Waziri anaehusika. Aidha, kazi ya kupitia upya mikataba yote iliyokwisha kutolewa ya ukodishaji wa visiwa au sehemu yake tayari imekamilika ambapo idadi ya mikataba kumi imefanyiwa mapitio, kati yake mitatu inahusisha kukodisha kisiwa kizima (full lease) na saba inahusiana na ukodishwaji wa sehemu tu ya visiwa (part lease). Matokeo ya hatua hii yatapelekea Serikali kukusanya jumla ya USD 93,256 kwa mwaka.

V. UTEKELEZAJI HALISI WA MATUMIZI YA SERIKALI JULAI 2019 HADI MACHI 2020

51. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho cha mapitio, matumizi halisi ya Serikali yalifikia TZS 810.2 bilioni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya kutumia jumla

ya TZS 1,038.2 bilioni. Kati ya matumizi hayo, TZS 563.2 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida, sawa na asilimia 94 ya makisio ya TZS 600.3 bilioni. Kwa upande wa kazi za maendeleo, jumla ya TZS 246.9 bilioni zilitumika sawa na asilimia 56 ya makisio ya TZS 437.8 bilioni, ambapo kati ya fedha hizo, TZS 115.3 bilioni zinatokana na mapato ya ndani na TZS 131.6 zinatokana na Ruzuku na Mikopo kutoka nje .

i. Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu

52. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hicho cha miezi tisa jumla ya TZS 122.9 bilioni, sawa na asilimia 97 ya makadirio ya kipindi hicho ya TZS 127.1 bilioni zilitumika kwa huduma mbalimbali kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali. Matumizi hayo yameelekezwa katika mambo yafuatayo:

a. Malipo ya Kiinua Mgongo TZS 20.44 bilioni kwa wastaafu 874 na Pencheni ya TZS 20.79 bilioni kwa wastaafu 13,000 kwa mwezi;

b. Malipo ya Mikopo ya ndani na Riba ni TZS 12.4 bilioni;

c. Matumizi mengine ya Serikali kupitia Mfuko Mkuu TZS 68.5 bilioni;

d. Madeni ya Wazabuni TZS 0.7 bilioni.

ii. Matumizi ya Mfuko wa Miundombinu

53. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Mfuko wa Miundombinu, jumla ya TZS 41.0 bilioni zilipangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi kumi na saba (17). Katika kipindi cha miezi tisa, jumla ya TZS 21.2 bilioni zimetumika kutoka Mfuko wa Miundombinu kwa kugharamia miradi 15 sawa na asilimia 52 ya makisio ya mwaka mzima.

a) Deni la Taifa

54. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu deni inalodaiwa ili kuepuka kuingia deni kubwa lisilolipika. Hadi kufikia Machi 2020, Deni la Taifa limefikia TZS 817.98 bilioni likiwemo TZS 665.27 bilioni kutoka nje, sawa na asilimia 81.3 ya deni lote ambapo kati yake, asilimia 95.8 limedhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kiasi kilichobakia cha TZS 152.7 bilioni ni deni la ndani, sawa na asilimia 18.7 ya deni lote ambapo deni kutokana na Hatifungani ni TZS 108.15 bilioni, ZSSF ni TZS 42.6 bilioni na PBZ ni TZS 1.9 bilioni.

55. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia misingi ya usimamizi bora wa fedha za umma kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 5 cha Sheria ya Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016, mikopo yote imetumika kwa kazi za maendeleo. Aidha, kwa kuzingatia deni la

TZS 817.98 bilioni na Pato la taifa la TZS 3,978 bilioni, uwiano wa deni kwa Pato la Taifa umefikia asilimia 26.6, kabla ya kuzingatia thamani halisi ya deni kwa miaka ijayo (Net Present Value). Kiwango hicho cha uwiano wa deni kwa Pato la Taifa ni cha chini mno ikilinganishwa na ukomo wa assilimia 50, unaotumika kama kigezo kimojawapo cha uhimilivu wa deni. Kwa muktadha huo, bado deni letu ni himilivu kwa vigezo vya Kimataifa.

VI. MATARAJIO YA MAPATO KWA MWAKA 2019/2020

A. Matarajio ya Mapato ya Ndani Julai – Juni 2019/2020

56. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo katika kipindi cha Julai hadi Machi 2020, mapato ya Serikali yanatarajiwa kufikia TZS 1,118.8 bilioni. Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 835.3 bilioni sawa na asilimia 85.5 ya makadirio ya awali. Hata hivyo, utendaji huo ni sawa na ukuaji wa asilimia 11.5 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka uliopita. Kwa upande wake, Ruzuku na Mikopo kutoka Washirika wa Maendeleo zinatarajiwa kuingiza TZS 283.5 bilioni, ambapo Ruzuku ni TZS 72.7 bilioni na mikopo ni TZS 210.8 bilioni.

57. Mheshimiwa Spika, Mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 713.0 bilioni, sawa na asilimia 83.0 ya bajeti ya TZS 859.7 bilioni, ambapo ni sawa na ukuaji wa asilimia 6.2 ikilinganishwa na TZS 671.4 bilioni zilizokusanywa mwaka wa fedha uliopita, 2018/2019. Kati ya kiasi hicho, matarajio ni kuwa TRA itakusanya TZS 286.2 bilioni sawa na asilimia 81.7 na hivyo makusanyo yake kushuka kwa asilimia 0.8 ikilinganishwa na TZS 288.5 bilioni zilizokusanywa mwaka wa fedha uliopita. Kwa upande mwengine, ZRB inatarajiwa kukusanya asilimia 83.1 ya lengo sawa na TZS 405.8 bilioni ikimaanisha ukuaji wa asilimia 12.3 kutoka makusanyo halisi ya TZS 361.4 bilioni kwa mwaka wa fedha uliopita. Kodi ya Mapato kutoka Serikali ya Muungano inatarajiwa kufikia TZS 21.0 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo.

58. Mheshimiwa Spika, kwa mapato ya mawizara na mengine yasiyokuwa ya kodi, matarajio ni kuvuka lengo kwa asilimia 4.7 kwa kukusanya TZS 122.3 bilioni na hivyo kupelekea ukuaji wa asilimia 57.0 ikilinganishwa na ukusanyaji wa TZS 77.9 bilioni zilizopatikana katika mwaka wa fedha 2018/2019. Matarajio hayo yanaanshiria utendaji ufuatao:

i. Mapato ya Mawizara yatafikiaTZS 105.7 bilioni sawa na asilimia 106.4 ya makadirio ya mwaka ya TZS 99.33 bilioni;

ii. Gawio la Mashirika ya Serikali ni TZS 5.6 bilioni sawa na asilimia 70.0 ya makadirio ya mwaka ya TZS 8.0 bilioni; na

iii. Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, linatarajiwa kufikia TZS 11.25 bilioni sawa na asilimia 115.8 ya makadirio ya mwaka ya TZS 9.5 bilioni.

Mfuko wa Miundombinu

59. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, matarajio ya mapato ya Mfuko wa Miundombinu ni TZS 34.1 bilioni sawa na asilimia 83.2 ya makadirio ya Bajeti. Pamoja na kutofikia lengo, kiwango hicho cha ukusanyaji kinaashiria ukuaji wa mapato ya kianzio hiki kwa asilimia 8.3 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Kitaasisi, TRA inatarajiwa kukusanya TZS 10.8 bilioni na ZRB inatarajiwa kukusanya TZS 23.3 bilioni.

B. Matarajio ya Matumizi Julai 2019-Juni 2020

60. Mheshimiwa Spika, hadi kumalizika mwaka wa fedha 2019/2020, matumizi ya Serikali yanatarajiwa kufikia TZS 1,158.8 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 81.6 ya Bajeti ya mwaka ya TZS 1,419.4 bilioni. Jumla ya TZS 740.0 bilioni zitatumika kwa matumizi ya Kazi za Kawaida kwa mchanganuo ufuatao:

i. Matumizi ya Mishahara yanatarajiwa kufikia TZS 363.8 bilioni ambapo TZS 248.3 bilioni kwa Wizara

na Taasisi zenye Mafungu, sawa na asilimia 82.4 ya bajeti ya mwaka. Kutofikiwa matarajio ya matumizi ya mishahara kunatokana na uamuzi wa Serikali uliotokana na mripuko wa maradhi ya COVID-19, wa kuakhirisha ulipaji wa nyongeza maalum za mishahara zilizopangwa kupewa kuanzia mwezi wa Aprili 2020. Aidha, jumla ya TZS 115.5 bilioni zimetumika kulipa mishahara ya Taasisi zinazopokea Ruzuku, sawa na asilimia 106.8 ya bajeti ya mwaka;

ii. Jumla ya TZS 373.4 bilioni ni Matumizi Mengineyo ya kuendeshea Ofisi ambapo kwa Wizara na taasisi zenye Mafungu ni TZS 148.8 bilioni sawa na asilimia 88.3 ya makadirio ya mwaka wakati kwa Taasisi zinazopokea Ruzuku, matumizi halisi yanatarajiwa kufikia TZS 72.3 bilioni, sawa asilimia 74.0 ya makadirio ya mwaka; na

iii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali yanatarajiwa kufikia TZS 152.3 bilioni, sawa na asilimia 96.3 ya makadirio ya mwaka mzima.

61. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, hadi kufikia Juni 2020 inatarajiwa kuwa jumla ya TZS 418.8 bilioni zitatumika, sawa na asilimia 72.6 ya makadirio ya awali. Kati ya matumizi hayo, TZS 135.3 bilioni ni kutokana na fedha za ndani, sawa na asilimia 74.2 ya makadirio

na TZS 283.5 bilioni ni Mikopo na Ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 71.8 ya makadirio ya TZS 394.6 bilioni.

VII. MRIPUKO WA MARADHI YA COVID-19 NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

62. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa tarehe 9 mwezi huu nikiwasilisha hotuba ya mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka ujao wa fedha, ambayo Baraza lako tukufu liidhinisha tarehe 10 Juni. Katika hotuba yangu hiyo, niliahidi kutoa maelezo zaidi ya athari ya maradhi ya COVID-19 hapa nchini na hatua zilizochukuliwa na za ziada zitazochukuliwa na Serikali nitapowasilisha Hotuba hii ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2020/2021. Kwa hivo naomba uniruhusu nitimize ahadi yangu hiyo.

63. Mheshimiwa Spika, katika nchi nyingi maradhi ya corona yalianza na athari katika sekta ya afya na hatimae katika maeneo ya kiuchumi na kijamii, kinyume na kwetu ambako yalianza na athari ya kiuchumi na baadae zikafuata za afya. Athari zilitokana na hatua tulizozichukua kuihami jamii yetu dhidi ya kuambukizwa na maradhi hayo. Tumezingatia mapendekezo yaliyotolewa na watu na sekta mbalimbali juu ya hatua za kuchukuliwa na Serikali yakiwemo ya kuzuia

watu kutoka nje muda wote (lockdown) au hata muda maalum (curfew), kuzuia usafiri baina ya Unguja na Pemba na baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, na pia kuweka karantini ya watu kwenda nje ya Mkoa wanaoishi.

64. Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Ali Mohamed Shein, na kwa mashirikiano makubwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi imara wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Serikali iliona kuwa hali yetu haikufikia kuchukuliwa hatua hizo kubwa ambazo athari zake kijamii na kiuchumi ni kubwa sana. Miongoni mwa hatua ambazo Serikali ilizichukua kwa haraka ni hizi zifuatazo:

i. Kupiga marufuku mikusanyiko yote ikiwemo mikutano, semina, michezo, kumbi za starehe na kufunga skuli zote kuanzia za maandalizi hadi sekondari, vyuo vya elimu ya juu na madrasa;

ii. Kuelekeza kufuatwa kwa maelekezo ya wataalamu wa afya ikiwemo ya kuosha mikono kwa maji yanayotiririka, kutumia vitakasa mikono, kuzingatia masafa baina ya mtu na mtu na baadae, uvaaji wa barkoa; na

iii. Kuzuia ndege za watalii wa makundi kutoka Italy, baadae na nchi nyengine zote, kuweka wasafiri wanaoingia nchini katika uangalizi wa lazima wa

siku 14 na hatimae kuzuia wasafiri wote kutoka nje kuingia nchini.

65. Mheshimiwa Spika, hatua nyengine zilizochukuliwa ni hizi zifuatazo:

iv. Kuandaa Mpango maalum wa Kujitayarisha na Kukabiliana na maradhi hayo (COVID-19 Preparedness and Response Action Plan);

v. Kuandaa Mpango wa Kufufua Uchumi baada ya kumalizika maradhi hayo (Economy Recovery Plan);

vi. Kuanzisha Mfuko maalum wa kupokelea michango kwa ajili ya kukabiliana na maradhi hayo ambapo hadi tarehe 8 Juni jumla ya TZS 1,376.6 milioni zilikusanywa kutoka watu, mashirika na taasisi mbalimbali; na

vii. Kusimamia kwa karibu zaidi mapato na matumizi ya Serikali kulingana na hali ya fedha ilivyo Serikalini baada ya kupungua kwa mapato.

66. Mheshimiwa Spika, kimsingi, jitihada za Serikali kwa kuanzia zililenga katika maeneo mawili makubwa, mosi kuhakikisha wananchi wanakingwa na maambukizo ya maradhi hayo ya corona na, pili, kuhakikisha kuwa Serikali inaendelea kutoa huduma za msingi

kwa wananchi wake ikiwemo mahitaji zaidi ya sekta ya afya. Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo bado maradhi hayo yaliingia nchini kwetu ambako jumla ya watu 134 walibainika kuathiriwa na maradhi hayo katika kipindi hicho na 6 kati yao wakafariki dunia. Hatua za kukabiliana na maradhi hayo zilipelekea kuathirika kwa Bajeti ya Serikali, kwa upande mmoja kutokana na kupungua mapato na, kwa upande mwengine, kwa kulazimika kuelekeza matumizi mengi katika hatua za kukabiliana na maradhi hayo, ikiwemo kuhudumia vituo vitano vilivyofunguliwa kwa kuhudumia wagonjwa waliobainika.

67. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchumi, baadhi ya athari za maradhi hayo ni kama ifuatavyo:

i. Kusita kuja kwa watalii nchini;
ii. Kuathirika sana mwenendo wa biashara na wawekezaji ambao wamekosa mapato kipindi chote hiki;
iii. Kuathirika kwa ajira na kipato kwa wafanyakazi walio wengi katika sekta ya utalii na wanaowategemea;
iv. Kujitokeza uhaba wa fedha za kigeni, ulioathiri biashara hasa ya uingizaji bidhaa, kwa baadhi ya benki za biashara na baadae utoaji mkubwa wa amana za Shilingi ili kuwezesha ununuzi wa Dola za Marekani katika Benki nyengine;
v. Kupungua kwa zaidi ya nusu mapato ya Serikali,

ya ndani na nje, kulikopelekea kutumika zaidi fursa ya kutumia zaidi (overdraft) ambayo ina gharama; na

vi. Kuathirika sana kwa matumizi ya Serikali kwa sababu ya uhaba wa mapato kulikopelekea kutotekelezwa kwa baadhi ya shughuli na miradi iliyopangwa katika robo ya mwisho ikiwemo dhamira ya serikali ya kupandisha mishahara kwa baadhi ya makundi maalum ambayo hayakunufaika na nyongeza za kabla.

68. Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali na wananchi zikiwemo za kuomba sana nusura ya Mwenyezi Mungu, kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya na ya Serikali zinaelekea kuzaa matunda kwani hali ya maradhi imeweza kupungua bila ya kuleta athari kubwa za kijamii tofauti na tulivoshuhudia katika nchi nyengine. Nachukua fursa hii kumshukuru kwa dhati mola wetu muumba na muweza kwa kuendelea kutulinda na kutuhifadhi waje wake. Nilianza kwa kumshukuru kwa neema zake kubwa na ndogo; hifadhi yake hii ni sehemu ya neema zake hizo tunazoshukuru sana. Tuendelee kuomba sana hifadhi ya mola wetu muumba.

69. Mheshimiwa Spika, Mpango wetu wa Kuhuisha Uchumi (ERP) baada ya athari za corona kimsingi unalenga kuhakikisha kuwa ***wote tuwe*** salama – wote tukimaanisha kuwa *Serikali ibaki salama* - na

uwezo wake wa kuhudumia wananchi na kugharamia maendeleo. Aidha, *biashara na uwekezaji ubaki salama* - na ziweze kuendelea baada ya kumalizika maradhi ya corona na pia *watu wawe salama* – wasiambukizwe na virusi vya corona na waendelee kuwa na ajira na kujipatia rizki zao za halali. Maeneo makuu katika Mpango huo ni pamoja na haya yafuatayo:

i. Kuhuisha Utalii

70. Mheshimiwa Spika, kwa miaka zaidi ya 20 sasa Utalii umejitokeza kuwa sekta muhimu kwa uchumi wetu, sio tu kwa mchango wake wa moja kwa moja katika Pato la Taifa, bali pia katika kuziimarisha sekta nyengine kwa kuzipatia soko la bidhaa na huduma zake, kama vile Kilimo, uvuvi, biashara za bidhaa mbalimbali, mikahawa na huduma nyengine. Chini ya ERP, miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa kufufua utalii ni kuimarisha miundombinu yetu kama vile kiwanja cha ndege na bandari ili iendane na mahitaji ya kulinda watalii dhidi ya corona, kusimamia utekelezaji wa Utaratibu Maalum wa watoa huduma kwa utalii (standard Operating Procedure – SOP). Serikali pia itashirikiana na Sekta binafsi kuandaa program maalum za pamoja za kuitangaza Zanzibar katika masoko ya utalii na kutoa vivutio maalum.

ii. Kuendeleza biashara

71. Mheshimiwa Spika, tokea katikati ya miaka ya 1980 Serikali ilipofungua milango ya biashara kwa sekta binafsi, Zanzibar imejitokeza kuwa kituo muhimu cha biashara za kuingizwa na kusafirishwa. SMZ inathamini sana mchango wa wafanyabiashara katika uchumi wa Zanzibar, mapato ya serikali na ajira kwa wananchi waliowengi. Katika kipindi hiki cha athari za corona, haja ya kuendelea kuwasadia wafanyabiashara inajitokeza zaidi ili kupunguza pengo lililoachwa na utalii, kunusuru kushuka zaidi mapato ya Serikali, na kusaidia ajira na kipato cha watu binafsi. Biashara hizo zinalenga kuhakikisha upatikanaji wa chakula, dawa, vifaa vya ujenzi na bidhaa nyengine muhimu. Serikali itachukua hatua maalum ikiwemo, kwa kushirikiana na Benki Kuu, kuhakikisha kunakuwepo kwa fedha za kigeni za kufanikisha biashara hiyo kuziba pengo lilioachwa na upungufu wa mapato ya utalii.

iii. Kuimarisha Kilimo na Uvuvi

72. Mheshimiwa Spika, sekta ndogo za asili za kilimo na uvuvi nazo ni muhimili mkuu kwa jamii yetu. Hata wakati huu wa athari za corona, baadhi ya wananchi wenzetu ambao ajira zao zimeathiriwa na maradhi hayo walilazimika kuhamia kwenye sekta hizo na kutumia ujuzi wao wa asili ili kujikimu na kipato. Athari ya corona kwa sekta ndogo hizi sio ya moja

kwa moja bali imejitokeza katika kupungua kwa soko la bidhaa za sekta ndogo hizo kulikopelekea kupungua pia kwa bei zake na hivyo kumuumiza mkulima na mvuvi. Katika kipindi kifupi, Serikali imesaidia sekta ndogo ya kilimo kupata matrekta maalum ya kulimia katika mabonde yenye maji (rotavators) na kusaidia wakulima wa mpunga katika mabonde mbalimbali.

73. Mheshimiwa Spika, Serikali imesaidia pia Kilimo cha mazao mengine ya chakula, hasa ya aina ya mizizi kama vile mihogo na viazi vidogo, kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa chakula nchini na wa kipato kwa wakulima hao. Kwa mpango wa muda mrefu, azma ni kuhakikisha kuwepo kwa soko la bidhaa hizo hapa nchini, hususan kutumika kwake kama malighafi katika usarifu viwandani.

iv. Kusaidia Biashara kujikwamua na athari za maradhi ya corona

74. Mheshimiwa Spika, ERP ina sehemu pia ya namna ambavyo sekta ya fedha kupitia benki nchini itakavyosaidia biashara na wawekezaji katika kipindi hiki. Serikali imeshirikiana na Benki Kuu ambayo hatimae imechukua hatua za kuimarisha upatikanaji wa fedha katika mabenki na kwa gahrama nafuu. Miongoni mwa hatua nyengine, Benki Kuu imeshusha kiwango cha lazima cha mabenki kubakisha Benki Kuu (Stratutory Minimum Reserve – SMR) na pia kiwango

cha riba inachotoza benki zinapokopa kwake (discount rate). Hatua ya kushusha SMZ imelenga katika kuongeza ukwasi katika mabenki wakati ushushaji wa "discount rate" umelenga katika kushusha gharama ya mabenki kukopa nayo kukopesha. Serikali pia imetenga fedha maalum za kusaidia biashara mbalimbali kupata mikopo nafuu.

v. Kusimamia vyema Mapato na matumizi ya Serikali

75. Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua maalum za kuchunga mapato na matumizi yake katika kipindi hiki, kwa kupokea na kujadili taarifa ya hali ya fedha Serikalini kila mwezi. Taarifa hizi zililenga kuitaarifu Serikali juu ya mwenendo wa mapato yake ili ikubaliane na hatua zinazotekelezwa za kudhibiti matumizi ili kunusuru hali kuwa mbaya zaidi.

vi. Kutoa unafuu katika Mfumo wa Kodi

76. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika mapendekezo ya Serikali ya hatua za kuimarisha mapato, kuna hatua kadhaa zilizolenga kurekebisha mfumo wa kodi ili kumpunguzia mzigo mfanyabiashara na muwekezaji. Miongoni mwa hatua hizo ni: (i) kupandisha kiwango cha mauzo cha mtu kulazimika kujisajili na VAT kutoka Shilingi 30 milioni hadi milioni 50; (ii) Kushusha kiwango cha VAT kutoka asilimia 18 hadi asilimia 15. Ushushaji huu umekwenda sambamba

na marekebisho kama hayo kwenye Sheria ya Ushuru wa Mahoteli.

77. Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Oktoba mwaka jana nchi yetu pia ilikabiliwa na mvua za muda mrefu zilizokutana na vuli na masika. Neema hiyo ya mvua imeleta unafuu katika upatikanaji na bei kwa baadhi ya mazao japokuwa pia imeathiri baadhi ya maeneo hasa kwa makaazi ya wananchi na miundombinu. Wakati tunaendeela kutoa pole kwa walioathirika, kwa ujumla tunamshukuru Allah kwa neema zake zote hizo.

VIII. MWELEKEO WA BAJETI 2020/2021-2022/2023

78. Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, maendeleo yetu yanategemea ukuaji na mageuzi ya uchumi wetu na jinsi ukuaji huo unavonufaisha wananchi walio wengi, hasa wa kipato cha chini. Kwa bahati mbaya, uchumi wetu umeathiriwa na maradhi ya corona na hivyo matarajio ni kuwa kasi ya ukuaji wa uchumi itapungua kutoka matarajio ya awali ya ukuaji wa asilimia 7 hadi nane na kufikia ukuaji wa baina ya asilimia 3 na 5, kutegemea zaidi na kasi ya kufufuka utalii. Kwa sababu hii, tunapaswa kuchukua jitihada maalum za kutekeleza kwa vitendo Mpango wetu wa kuhuisha uchumi. Kupitia Mpango huo, Serikali imeweka hatua makhsusi (recovery package) za kusaidia Sekta ambazo zimeathirika zaidi kwa maradhi hayo.

79. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hiyo ya athari za corona na azma yetu ya kutekeleza Mpango wa kuhuisha uchumi, shabaha na malengo ya uchumi kwa kipindi cha miaka mitatu ni kama ifuatavyo:

a) Kuhakikisha kuwa uchumi unahuika na unaendelea kukua japo kwa kasi ndogo ya baina ya asilimia 3 mpaka 5;
b) Kuendeleza jitihada za mageuzi ya uchumi kwa kuimarisha zaidi uzalishaji viwandani, huduma mbalimbali ikiwemo utalii, kutumia zaidi rasilimali za bahari (uchumi wa buluu) kwa kuiarisha uchumi na kuendeleza uimarishaji wa sekta ya Kilimo; na
c) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kuwa wastani wa chini ya asilimia 5.

80. Mheshimiwa Spika, shabaha nyengine ni kama ifuatavyo:

d) Kuimarisha zaidi ukusanyaji wa mapato ya ndani na kufikia wastani wa asilimia 25.2 ya Pato la Taifa kutoka asilimia 23.6 kwa mwaka 2018/2019;
e) Kuendelea kuwa na kiwango kidogo cha utegemezi katika Bajeti kwa sehemu yake kubwa kugharamiwa kwa mapato ya ndani; na
f) Kuendelea kuhakikisha kuwa Matumizi ya Serikali yanaendana na mapato na kudhibiti nakisi. Aidha, kwa kadiri itavyowezekana sehemu ya matumizi kwa kazi za maendeleo izidi kuimarika.

81. Mheshimiwa Spika, Faida zinazopatikana kutokana na kukua kwa uchumi zitaendeela kunufaisha wananchi kupitia huduma mbalimbali za jamii kama elimu, afya, maji safi na salama na mazingira bora ya kuishi.

Makadirio ya Mapato

Mapato ya Ndani

82. Mheshimiwa Spika, pamoja na athari za corona, Serikali imeamua kuendelea na makadirio ya mapato na matumizi kwa mtazamo wa matumaini. Mtazamo wa Serikali ni kuwa athari za corona ni jambo la muda na la kupita, ikiwemo kwenye uchumi na mapato ya Serikali. Kwa mustakabali huu, jumla ya TZS 1,050 bilioni zimekadiriwa kukusanywa kwa mwaka 2020/2021 kutokana na vyanzo vya ndani. Kati ya makadirio hayo, mapato kutokana na kodi ni TZS 921.3 bilioni wakati mapato yasiyo ya kodi yamekadiriwa kufikia TZS 128.7 bilioni.

Makadirio ya Ukusanyaji Kitaasisi

83. Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, makadirio haya hugawanywa kwa taasisi zetu za ukusanyaji na kuwa ndio malengo yao ya utendaji. Kwa mwaka ujao wa fedha, mgao wa makadirio hayo kwa TRA ni TZS 383.5 bilioni. ZRB imekadiriwa kukusanya TZS 516.7 wakati Wizara zetu zimekadiriwa kukusanya TZS 128.7 bilioni, ikiwemo ada zinazotozwa na Wizara

mbalimbali za jumla ya TZS 104.7 bilioni, gawio la faida inayokadiriwa kupatikana katika Mashirika ya SMZ ni TZS 10.5 bilioni na gawio kutokana na faida ya Benki Kuu ni TZS 13.5 bilioni. Bado inatarajiwa kupokea TZS 21.0 bilioni kama kodi ya mapato kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar.

Ruzuku na Mikopo kutoka Nje

84. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kugharamia maendeleo yake kwa kutumia pia mikopo na ruzuku kutoka nje ya nchi. Kwa mwaka 2020/2021, inatarajiwa kupokea jumla ya TZS 423.2 bilioni kutokana na Ruzuku na mikopo. Kati ya kiasi hicho, jumla ya TZS 340.5 inatarajiwa kupokelewa kama mkopo na TZS 82.7 bilioni ni ruzuku. Katika kiasi hicho cha mikopo, TZS 61.0 bilioni zinatarajiwa kupatikana kama marejesho kutoka Benki ya Exim ya China, kwa mujibu wa makubaliano yetu, ikiwa ni kiasi ambacho SMZ imetumia katika ujenzi wa jengo jipya la abiria katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume. Inatarajiwa kwamba masuala yote ya mkopo wa ziada kutoka Benki hiyo yatakamilishwa baina yake na SMT na hivyo kuwezesha marejesho hayo.

Mwelekeo wa Matumizi

85. Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji ya kazi za kawaida na maendeleo, kwa mwaka ujao wa fedha

Serikali inatarajia kutumia jumla ya TZS 1,579.2 bilioni kama ifuatavyo:

i. Matumizi ya Kazi za Kawaida ni TZS 969.3 bilioni, kwa mgawanyo ufuatao:
   a. jumla ya TZS 440.6 bilioni ni kwa ajili ya kulipa mishahara, ikiwemo ya mawizara na Mafungu mengine ya Bajeti ya TZS 316.8 bilioni na ile ya taasisi zinazopokea Ruzuku ya TZS 123.8 bilioni;
   b. Kiasi kilichobakia cha TZS 290.8 bilioni ni kwa ajili ya matumizi ya kuendeshea ofisi (other charges – OC), ikiwemo TZS 182.6 bilioni kwa ajili ya Wizara na taasisi zenye Mafungu na TZS 108.2 bilioni ni kwa taasisi zinazopokea Ruzuku; na
   c. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ni TZS 237.9 bilioni.
ii. Matumizi ya Kazi za Maendeleo ya TZS 609.9 bilioni.

86. Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina ya matumizi ya Kazi za Maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha niliyatoa asubuhi ya leo wakati nikiwasilisha Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2020/2021. Hivyo sikusudii kurejea tena maelezo yale kwani Hotuba zangu hizi mbili zinapaswa kusomwa kwa pamoja. Pamoja na hivo, naomba nisisitize tu mambo yafuatayo katika matumizi hayo ya maendeleo:

i. Kwanza, kwamba Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya umalizaji wa jengo la abiria (Terminal 3) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume. Hadi sasa mradi unaendelea vyema na matarajio ni kukamilika mwishoni mwa robo ya kwanza ya mwaka mpya wa fedha zaidi ya asilimia 70 za ujenzi umekamilika;

ii. Serikali itaanza rasmi ujenzi wa barabara ya zamani ya Wete – Chake kwa kiwango cha lami na hivyo kukamilisha ahadi yake ya muda mrefu kwa wananchi wa Pemba wanaoitumia barabara hiyo. Kwa niaba ya Serikali, niruhusu niwashukuru sana wananchi wote wa Pemba hasa wanaoishi na kuitumia barabara hiyo kwa ustahamilivu wao na kuendelea kuiamini Serikali yao. Nawaambia tu kuwa changamoto kuu zilizokwamisha kujengwa barabara hiyo sambamba na zile za Wete – Konde na Wete – Gando kwa sasa zimemalizika na barabara itaanza kujengwa hivi karibuni;

iii. Serikali pia itaanza kutekeleza mradi mwengine uliokuwa umekwama kwa muda mrefu, wa ukarabati mkubwa wa hospitali za Mnazimmoja, Mwembeladu na Kidongochekundu. Fedha kwa ajili ya mradi huu US 42.8 kutoka Saudi Fund, Kuwait Fund, BADEA na SMZ yenyewe zimepatikana nazo zipo tayari;

iv. Pia, kwa furaha kubwa, natamka kuwa Serikali itaendeleza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa

hospitali mpya ya rufaa na kufundishia hapo Binguni. Tayari Serikali imeshaanza matayarisho ya kuanza ujenzi kwa pesa zake yenyewe na sasa imepata nguvu zaidi kutokana na mkopo nafuu kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Saudi (Saudi Fund), wa Kuwait (Kuwait Fund) na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu na Afrika (BADEA) US 33.5 milioni zimepatikana;

v. Serikali pia imetenga jumla ya TZS 7.0 bilioni kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kufufua Uchumi;
vi. Kuendeleza ujenzi wa Mahkama Kuu mpya Tunguu;
vii. Kuendeleza ujenzi wa barabara kadhaa, Unguja na Pemba; na
viii. Kuendelea na matayarisho na ujenzi wa bandari mpya ya Mpigaduri.

87. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya Mfuko wa Miundombinu jumla ya TZS 44.2 bilioni zimetengwa kwa ajili ya kugharamia miradi maalum ya maendeleo kwa mwaka 2020/2021. Uchambuzi wa miradi hiyo unaonekana katika **Viambatanisho.**

IX. MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO

88. Mheshimiwa Spika, ili kufikia matarajio ya ukusanyaji na kuimarisha mazingira ya uwekezaji na biashara

nchini, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali inakusudia kuchukua hatua kadhaa za kurekebisha Sheria mbalimbali. Kwa upande mwengine, bado Serikali bado itaendeleza Sera yake ya kutopandisha kodi katika vyanzo vyake vya ndani badala yake kutegemea zaidi kuimarika kwa uchumi, uwajibikaji katika kulipa kodi na ufanisi wa taasisi zetu za kodi katika kufikia malengo yaliyowekwa ili kutimiza azma ya Chama chetu Cha Mapinduzi, ya kujenga Taifa linalojitegemea badala ya kuendeshwa kwa ruzuku kutoka nje ya nchi.

89. Mheshimiwa Spika, Miongoni mwa hatua zinazopendekezwa kuchukuliwa ili kuimarisha mfumo wa kodi nchini ni pamoja na hizi zifuatazo:

i. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)

a. Kupunguza Kiwango cha VAT

90. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na athari ya COVID -19 katika uchumi, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021 inapendekeza kupunguza kiwango cha kutozea Kodi ya Ongezeko la Thamani kutoka asilimia 18 hadi asilimia 15.

b. Kutoa Msamaha wa VAT kwenye Vifaa vya Uvuvi

91. Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta za asili hapa nchini, kama ilivyo kilimo cha mazao, na inayoajiri na kuwa chanzo kikuu cha mapato kwa wananchi wengi na hivyo kusaidia juhudi zao za kujikwamua na umaskini.

92. Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua jitihada za kuimarisha shughuli za uvuvi, ikiwemo kuanzisha Kampuni yake ya Uvuvi (ZAFICO). Ili kuwasaidia zaidi wavuvi, Serikali inapendekeza kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa vifaa vya uvuvi ikiwemo boti kubwa za kuanzia urefu wa mita 18 na zaidi, mashine za boti, pamoja na vifaa vyengine vya uvuvi vinavyoingia nchini. Orodha kamili ya vifaa hivyo kwa mujibu wa "HS Codes" zake inaonekana katika Kanuni chini ya Sheria hiyo . Kwa upande wa boti, uamuzi wa kusamehe boti zenye urefu wa kuanzia mita 18 na zaidi unalenga kutoathiri ujuzi wa asili wa ujenzi wa ngarawa, mitumbwi na mashua za uvuvi ambao ni sehemu ya utamaduni wetu muhimu.

c. Kupandisha Kiwango cha Mauzo Ghafi kwa Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)

93. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa kuna usimamizi bora wa mfumo wa VAT, ni aghalabu kwa Sheria za kodi hiyo kuweka kiwango maalum cha mauzo

(threshhold) ili mfanyabiashara aweze kusajiliwa. Wafanyabiashara wote wasiofikia kiwango hicho huachwa nje ya mtandao wa kutoza na kukusanya VAT. Kwa sasa, ili mlipakodi asajiliwe kwenye VAT kwa hapa Zanzibar lazima awe na mauzo ghafi ya angalau Shilingi milioni 30 kwa mwaka. Kiwango hicho ni cha muda mrefu na hakiendani na mabadiliko makubwa ya kiuchumi yanayoendelea. Hivyo, Serikali inapendekeza kupandisha kiwango hicho cha mauzo kutoka Shilingi milioni 30 hadi Shilingi milioni 50 kwa mwaka. Hatua hii pia ni kwenda sambamba na mabadiliko yaliyopendekezwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuwa na kiwango cha chini cha USD 25,000 katika mfumo wa usajili wa VAT.

ii. Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli Na. 1 ya Mwaka 1995

94. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na athari ya COVID -19 katika uchumi, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021 inapendekeza kupunguza kiwango cha kutozea Ushuru wa Hoteli kutoka asilimia 18 hadi asilimia 12. Pendekezo hili limezingatia kuwa walipakodi wa Uashuru wa hoteli hawana fursa ya kujirejeshea VAT wanayolipa kwenye ununuzi wao hivyo ni gaharama kwao. Aidha, pendekezo hili linahusu tu walipakodi wanaolipia kodi kwa kiwango cha asilimia (ad valorem) na sio wanaolipia kwa kiwango maalum (specific) ambao kiwango chake hakitobadilika.

iii. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari Nam. 2 ya mwaka 1999 (The Port Service Charge Act no. 2 of 1999)

95. Mheshimiwa Spika, Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara katika sekta ya usafirishaji wa vyombo vya baharini juu ya thamani kwa ukokotoaji wa Ada ya usafirishaji wa Baharini (Sea Transport Charge) ambayo ikijumuisha ada nyengine za Bandari. Ili kurekebisha kasoro hiyo, na kuondoa utozaji kodi juu ya kodi, Serikali inapendekeza kuondoa Ada ya Bandari (Port Service Charge), kodi ya miundombinu na tozo ya Mamlaka ya Usafiri Baharini (Maritime Levy) katika thamani ya ukokotoaji wa ada ya usafirishaji wa baharini.

iv. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAPA) Nam. 7 ya mwaka 2009.

e. Kuongeza Kipengele cha Pingamizi za Kodi (tax objection) katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAPA) Nam. 7 ya mwaka 2009.

96. Mheshimiwa Spika, ili kuweka haki kwa walipakodi, Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAPA) inaruhusu mlipakodi kuweka pingamizi (objection) dhidi ya

makadirio ya kodi yanayotolewa na Kamishna. Kumekuwa na maombi mengi ya kutaka pingamizi hizo zihusishe pia na uamuzi mwengine wa Kamishna badala ya huo wa makadirio pekee. Kwa hivyo, Serikali inapendekeza kufanya mabadiliko katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAPA) nam. 7 ya mwaka 2009 kwa kuingiza utaratibu wote wa pingamizi (Objection) dhidi ya uamuzi wa Kamishna zaidi ya ule wa makadirio. Hata hivyo, ili kuepusha kutumika vibaya fursa hiyo, utaratibu wa pingamizi hizo utawekwa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha kwa kuutungia Kanuni.

b. Kumpa Uwezo Waziri Kuongeza Muda wa Kuwasilisha Ritani na Malipo ya Kodi Wakati wa Matukio Yasiyotarajiwa.

97. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAPA) Nam. 7, 2009, imebainisha siku ya mwisho ya uwasilishaji wa Ritani na malipo ya kodi kuwa ni tarehe 20 ya kila mwezi ya mwezi unaofuatia wa mauzo. Sheria kwa sasa imemruhusu tu Kamishna kuzingatia na kuweza kuruhusu ombi moja moja la kuongezewa muda lakini haikutoa fursa ya kuongezwa muda kwa walipakodi wengi kwa wakati mmoja pale inapoteka dharura ya kuhitaji hivyo. Hivyo, Serikali inapendekeza kurekebishwa kwa Sheria ili kumpa uwezo Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuongeza muda wa uwasilishaji wa ritani na ulipaji wa kodi ikiwa kutatokea dharura inayohitaji hali hiyo.

v. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Ajira Nam. 11 ya Mwaka 2005.

98. Mheshimiwa Spika, kwa sababu mbalimbali, Serikali imekuwa ikipokea maombi ya msamaha wa ada kwa vibali vya kazi wakati Sheria ipo kimya juu ya mamlaka hayo ya kusamehe. Hivyo, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005, kwa kutoa mamlaka kwa Waziri anaehusika na masuala ya Kazi kusamehe malipo ya ada ya vibali vya kazi baada ya kushauriana na kukubaliana na Waziri anaeshughulikia masuala ya fedha na kwa kuzingatia vigezo maalum vitakavyowekwa katika jadweli la Sheria hiyo. Hatua hii itasaidia katika kujenga uhalali wa misamaha, kudhibiti utoaji wake na kuhakikisha kuwa inatolewa tu kwa maslahi ya umma.

vi. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya mwaka 2016.

f. Udhibiti wa Utozaji wa Ada na Tozo

99. Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, kwa dhamira ya kuimarisha mazingira ya biashara nchini, Serikali imelazimika kufanya mapitio ya ada na tozo zinazotozwa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni mbalimbali. Katika mapitio hayo, imebainika kwamba tozo hizo ni nyingi mno, zinaleta mingongano kwa baadhi ya taasisi katika

usimamizi wake na baadhi yake zinakwaza uwekezaji na ufanyaji biashara na hivyo maendeleo ya kiuchumi. Ili kudhibiti hali hiyo, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nam.12 ya mwaka 2016 kwa kumpa uwezo Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha kupitia na kuidhinisha mapendekezo ya kuanzisha, kuongeza au kufuta Ada na Tozo. Aidha, kumpa uwezo wa kutoa miongozo juu ya usimamizi wake kwa Wizara na Taasisi kabla ya kuanza kutumiwa na taasisi husika.

c. Utowaji wa Risiti kwa Uwasilishaji wa Fedha za Mapato ya Serikali.

100. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam.12 ya mwaka 2016 imezitaka Wizara na Taasisi zote za Serikali zinazokusanya mapato kutokana na vyanzo mbalimbali kuwasilisha mapato hayo katika Wizara ya Fedha (Hazina). Kwa bahati mbaya, Sheria hiyo haikuweka wazi utaratibu wa kutoa risiti ambayo ni ushahidi wa upokeaji wa mapato yaliyowasilishwa. Ili kuondoa kasoro hiyo, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria hiyo kwa kuongeza kifungu kinachoweka utaratibu wa utoaji wa risiti kutokana na mapato yanayowasilishwa na Taasisi husika.

C. Kubadilisha Utaratibu wa Uzuiaji wa Mapato kwa Wizara na Taasisi za Serikali (Retention of Revenue)

101. Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuziachia baadhi ya taasisi mapato zinazokusanya kutokana na ada na tozo mbalimbali na pia, kwa baadhi yake, kuzipatia ruzuku. Utaratibu huu unaikosesha fursa Serikali kuwa na kumbukumbu sahihi za mapato yake yote. Katika kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato, Serikali inapendekeza kubadilisha utaratibu huo wa uzuiaji wa mapato bila ya taarifa zake kuingizwa kama sehemu ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Kuanzia sasa, matumizi kamili ya taasisi zote zinazopokea ruzuku kutoka Serikalini yataoneshwa kama sehemu ya matumizi ya Serikali kuu.

102. Mheshimiwa Spika, mapato yanayokusanywa na taasisi hizo yataoneshwa kama ni mapato ya Serikali kwa madhumuni ya Mfuko Mkuu wa Serikali lakini pia yatachukuliwa kuwa ni fedha zilizotangulizwa kutoka Hazina kwenda taasisi husika. Utaratibu huu unaojulikana kama *"Appropriation-in-aid"* unatarajiwa kuanza kutumika taratibu katika mwaka ujao wa fedha ili utumike kamili kuanzia mwaka 2021/2022.

D. Hatua za Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi

103. Mheshimiwa Spika, mbali ya hatua za marekebisho ya Sheria mbalimbali, hatua maalum za kiutawala zinatarajiwa kuchukuliwa ili kuimarisha uwezo wa taasisi zetu za kukusanya mapato kwa lengo la kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa ufanisi zaidi.

Miongoni mwa hatua hizo ni hizi zifuatazo:

i. Kupata taarifa kutoka kwa mtu wa tatu

104. Mheshimiwa Spika, kuimarisha na kuutumia vyema utaratibu wa kupata taarifa sahihi za wafanyabiashara kutoka kwa mtu wa tatu (third party) kupitia chombo kinachosimamia sekta husika (Regulatory Authority) badala ya kutegemea zaidi taarifa hizo kupitia kwa mfanyabiashara husika. Lengo la pendekezo hili ni kupata taarifa sahihi zitakazopelekea kukusanya kodi inayostahiki kwa mujibu wa Sheria. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa TZS 2,200 milioni.

ii. Kuharakisha Maamuzi ya Pingamizi za Kodi (Tax Objections)

105. Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa kutoa uamuzi dhidi ya pingamizi (tax objections) za

walipakodi unachelewasha pia ukusanyaji wa mapato ya Serikali. TRA itaandaa timu maalum ya kusimamia uharakishaji wa kutolewa uamuzi wa pingamizi za kodi kwa muda mfupi wa chini ya miezi mitatu. Pendekezo hilo linatarajiwa kukusanya kodi ya TZS 3,100 milioni.

iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi

106. Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea na jitihada zake za kuwajengea uwezo wafanyakazi katika fani mbalimbali. Mkazo maalum utawekwa katika fani ya Mafuta na Gesi Asilia ili kuwaongezea wafanyakazi ujuzi na maarifa ya kutoza kodi katika sekta hiyo mpya hapa Zanzibar ambapo harakati mbalimbali za utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia zinatarajiwa kuendelea nchini kwa mwaka mpya wa Fedha 2020/2021.

iv. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)

a. Kufanya Ukaguzi katika Hoteli za Kitalii

107. Mheshimiwa Spika, Serikali imeunda Kamati maalum kutoka wakuu wa Taasisi mbalimbali, chini ya uenyekiti wa Kamishna wa ZRB, ili kupitia ulipaji kodi wa hoteli na kugomboa kodi iliyokwepwa. Kamati hiyo inatarajiwa kukamilisha kazi yake katika robo ya kwanza ya mwaka ujao wa fedha kwa kupitia hatua mbalimbali ikiwemo zifuatazo:

a) Kufuatilia na kupata taarifa sahihi kwa kila hoteli pamoja na kuhakikisha kuwa Hoteli zote zinalipa kodi kwa kutumia viwango sahihi vilivyobainika na kuthibitishwa.
b) Kutumia mifumo ya kielektroniki ili kupata taarifa sahihi za huduma zinazotolewa katika hoteli, idadi ya wageni na siku ambazo wanakaa katika hoteli husika na malipo waliyofanya kwa huduma hizo.
c) Kutumia taarifa za hoteli na wageni kutoka kamisheni ya Utalii Zanzibar.

Hatua hii inatarajiwa kuingizia Serikali jumla ya **TZS 6.00 bilioni.**

b. Kufanya Ukaguzi wa Kodi Katika Sekta za Mawasiliano na Taasisi za Fedha.

108. Mheshimiwa Spika, Kufuatia makubaliano baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) ya kutumia taarifa za Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu (National Internet Data Centre – NIDC) katika ukusanyaji wa Mapato ya Serikali, ZRB inatarajia kufanya ukaguzi katika sekta za Taasisi za Fedha (benki) na sekta ya Mawasiliano ya Simu zinazotoa huduma hapa Zanzibar kwa lengo la kuhakikisha kodi sahihi imelipwa.Hatua hii inatarajiwa kuingizia Serikali jumla ya **TZS 2.5 bilioni.**

c. Kuondoa tofauti ya kodi kwa Mafuta ya "Bunker".

109. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa muda mrefu imeweka utaratibu wa kuwa na kiwango maalum cha kodi za Mafuta (Bunkering) yanayotumiwa na vyombo vya usafiri baharini vilivyosajiliwa Zanzibar. Hata hivyo, kumebainika udanganyifu kwa mafuta yanayotumika kwa mambo mengine kutajwa pia kama "bunker" ili kuweka kulipa kodi stahiki. Hivyo, Serikali inapendekeza kuondoa tofauti ya kodi kwa kulipisha Mafuta yote ya dizeli yanayoingizwa nchini kiwango sawa badala ya kuwa na kiwango maalum (kidogo) kwa mafuta ya bunker. Hatua hii inatarajiwa kuingizia Serikali jumla ya **TZS 0.90 bilioni.**

d. Kuanza rasmi Matumizi ya Mashine za Kielektroniki za Utoaji wa Risiti (VFD's)

110. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) iliamua kutumika mashine za kielektroniki za kutolea risiti (VFD's) wakati wa mauzo ya bidhaa au huduma ili kuwa na kumbukumbu sahihi za biashara makadirio ya kodi stahiki. Kwa sasa, tayari ufungaji wa vifaa (hardwarena utengenezaji wa programu (software) ya kuendeshea mfumo wa VFD's (VFDMS) vimekamilika. Matumizi ya machine hizo yanatarajiwa kuingizia Serikali jumla ya TZS 5.0 bilioni.

e. Kuendelea Kuwatambua na Kuwagawa Walipakodi katika Mfumo wa Maeneo.

111. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia ZRB ikishirikiana na TRA na Wakala wa Usajili wa Biashara (BPRA) ilianzisha utaratibu wa kugawa maeneo katika Mfumo wa Maeneo (Taxpayer Block Management System TBMS) na kuwatambua walipakodi kwa maeneo yao ya biashara na kurahisisha kusajiliwa kwao. Aidha, mfumo huu utarahisisha utambuzi wa maeneo yanayotakiwa kulipa kodi ya ardhi. Utaratibu huu ulianza kwa maeneo ya majaribio (Pilot Phase) ambayo ilihusisha maeneo ya Mlandege, Mwembeladu na Kwahajitumbo Unguja.

112. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 ZRB itakamilisha kazi za kuwatambua walipakodi wote Unguja na Pemba kwa kutumia mfumo huu na kuutumia rasmi kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Hatua hii inatarajiwa kuongeza wigo wa walipakodi kwa kusajili walipakodi wapya 500.

f. Kutoa Elimu kwa Walipakodi na Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi

113. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha uwajibikaji wa kulipa kodi kwa hiari ,elimu ya kodi itaimarishwa

zaidi kwa wafanyabiashara na wananchi kupitia vipindi vya Radio, Televisheni, kupitia mtandaoni, majarida, vipeperushi, semina na mikutano. Aidha, wafanyakazi wataendelea kuwajengewa uwezo zaidi kwa kuwapatia mafunzo ya kitaalamu katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba wanakwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi na teknolojia yanayoendelea kutokea duniani kote. Lengo la hatua hii ni kuimarisha ufanisi pamoja na kudhibiti mbinu mbalimbali zinazotumiwa na walipakodi wasiokuwa waaminifu katika kukwepa kodi.

114. Mheshimiwa Spika; Uchambuzi uliofanyika wa Mapitio ya Ada na Tozo zinazotozwa na Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa umepelekea Serikali kupendekeza kufuta, kupunguza au kuunganisha (harmonize) baadhi ya Ada na Tozo katika Sekta 8 za Kiuchumi ambazo zinawagusa wananchi, kama ifuatavyo:

115. Mheshimiwa Spika; Katika Sekta ya Biashara, Serikali inapendekeza hatua zifuatazo:

i Kufuta Tozo na Ada zote kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wa masokoni, mama lishe, waanika dagaa na jua kali za TZS 1,000 hadi 2,000 kwa siku wanachotakiwa kulipa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) . Wafanya biashara hao watalipa kiwango kimoja cha Ada

ya TZS 30,000 kwa mwaka na kupewa kadi maalumu ya usajili na utambulisho.

ii Kufuta Ada ya Mikataba ya Biashara ya asilimia 5 zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

iii Kufuta Leseni ya Ulinzi wa maadili na Sanaa ya TZS 50,000 inatozwa na Baraza la Sanaa na Sensa za Filamu (BASSFU)

iv Kupunguza Ada za usafi inayotozwa na LGA kutoka TZS 6,500 kwa mwezi (sawa na TZS 78,000 kwa mwaka) hadi TZS 50,000 mwaka, ambayo italipwa wakati wa kukata leseni.

v Kuweka viwango vya aina moja (specific amount) vya Leseni na Ada za usafi kwa kuzingatia vigezo vya mauzo na mtaji tofauti na ilivyo sasa. Aidha, malipo ya Leseni na Ada za usafi yatalipwa kwa pamoja wakati wa maombi ya leseni na yatakusanywa sehemu moja.

116. Mheshimiwa Spika; Katika Sekta ya Uwekezaji,Serikali inapendekeza hatua zifuatazo:

i Kufuta Ada ya uwekezaji ya asilimia 5% ya gharama za Uwekezaji inayotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

ii Kupunguza kiwango cha Ada ya Usajili wa Uwekezaji kinachotozwa Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) kutoka USD 500 hadi USD 200.

117. Mheshimiwa Spika; Katika Sekta ya Utalii, Serikali inapendekeza hatua zifuatazo:

i Kufuta Ada ya michezo ya baharini ya 5%-15% ya mauzo ya mwezi; Ada za Michezo ya baharini inayohusiana na michezo ya Vishada ya 10% ya mauzo; Ada ya Speed Boat ya 10% ya mauzo; Ada ya Jahazi ya 5% ya mauzo; Ada ya Kima Punju ya 15% ya mauzo; Ada ya Dolfin ya 5% ya mauzo na Ada ya Michezo mengine ya 10% ya mauzo zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

ii Kufuta Leseni za Maduka ya vitu vya Kitalii (yaliyo nje ya hoteli) zinazotolewa na Kamisheni ya Utalii. Aidha, Leseni hizo zitatolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuweka kiwango kisichozidi TZS 350,000 kwa mwaka kwa kuzingatia mauzo au mtaji wa duka.

iii Kupunguza kiwango cha Kibali cha Uhifadhi wa Bahari kinachotozwa na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi; kutoka kiwango cha TZS 6000 hadi 30,000 (kwa mwenyeji) na USD 100 hadi 500

(kwa Mgeni) na kuwa kiwango kimoja (specific amount) cha TZS 30,000 (kwa mwenyeji) na USD 500 (kwa Mgeni) na

iv Kuweka Viwango vya Ada ya Leseni vinavyotozwa na Kamisheni ya Utalii na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuwa vya aina moja (specific amounts) kwa kuzingatia vigezo vya madaraja, mauzo na mtaji. Aidha, malipo ya Leseni na Ada za usafi zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) yatalipwa wakati wa maombi ya leseni na yatakusanywa na Kamisheni ya Utalii.

118. Mheshimiwa Spika; Katika Sekta ya Usafirishaji Na Uagizaji, Serikali inapendekeza hatua zifuatazo:

i Kukusanya Ada na Tozo zote zinazotozwa na Taasisi zinazohusika na uingizaji na uondoshaji wa mizigo bandarini na kuziingiza katika mfumo wa Pamoja wa Kielektroniki wa Uondoshaji wa Shehena (Electronic Single Window System (eSWS) uliopo chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

ii Kufuta Tozo ya TZS 8000- 10000 kwa Kontena ya Futi 20 na Futi 40; Tozo la USD 0.2 kwa tani kwa mzigo mkubwa (bulk) na Tozo la TZS 5000 kwa gari inayotozwa na Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA).

iii Kufuta Tozo ya Ukaguzi wa ubora kwa vifaa vya utangazaji ya TZS 200,000 inatozwa na Tume ya Utangazaji kwa uingizaji wa TV tatu na kuendelea.

iv Kufuta Tozo ya USD 60 kwa mwaka ya Ruhusa ya Usalama wa kutumia Bandari, inayolipwa na Mawakala wa Forodha kwa Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA).

v Kupunguza kiwango cha Leseni ya Biashara inayolipwa na Mawakala wa Forodha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) kutoka TZS 300,000 hadi 1,000,000 na kuwa kiwango kimoja tu cha TZS 300,000.

119. Mheshimiwa Spika; Katika Sekta ya Viwanda, Serikali inapendekeza hatua zifuatazo:

i Kufuta Ada ya leseni ya TZS 500,000 hadi 3,000,000 kwa mwaka inayotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Viwanda vilivyosajiliwa na Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA).

ii Kufuta Ada ya Usafi kwa Viwanda vilivyosajiliwa na ZIPA ya TZS 10,000 hadi 100,000 kwa mwezi (sawa na TZS 120,000 hadi 1,200,000 kwa mwaka) inayotozwa na Mamlaka za Serikali

za Mitaa na kuweka kiwango kimoja cha TZS 600,000 kwa mwaka ambacho kitalipwa na wenye viwanda wakati wa ulipaji wa leseni.

iii Kufuta Ada ya Usafi kwa Viwanda visivyosajiliwa na ZIPA ya TZS 10,000 hadi 100,000 kwa mwezi (sawa na TZS 120,000 hadi 1,200,000 kwa mwaka) inayotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuweka kiwango kimoja cha TZS 240,000 kwa mwaka ambacho kitalipwa na wenye viwanda wakati wa ulipaji wa leseni.

iv Kuandaa muongozo wa pamoja utakautumiwa na Wakala wa chakula na Dawa (ZFDA), Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) Kamisheni Kazi (OSH) na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (CGCL) wakati wa ukaguzi wa ubora na usalama wa bidhaa zinazozalishwa Viwandani.

v Kuziunganisha Tozo za Uhakiki wa Mizani na Vipimo za TZS 25,000 hadi 60,000 kwa mizani/vipimo na Tozo za Uhakiki wa bidhaa zilizofungashwa za TZS 30,000 hadi 350,000 kwa bidhaa inayozalishwa; zinazotozwa na Wizara ya Biashara na Viwanda na kuweka kiwango kimoja cha Tozo cha TZS 300,000 kwa uhakiki wa mizani, vipimo na bidhaa zilizofungashwa.

vi Kuziunganisha Tozo za Uhakiki wa Mizani na Vipimo za TZS 10,000 hadi 60,000 kwa

mizani/vipimo na Tozo za Uhakiki wa bidhaa zilizofungashwa za TZS 30,000 kwa bidhaa inayozalishwa; zinazotozwa na Wizara ya Biashara na Viwanda na kuweka kiwango kimoja cha Tozo cha TZS 50,000 kwa uhakiki wa mizani, vipimo na bidhaa zilizofungashwa.

120. Mheshimiwa Spika; Katika Sekta ya Usafiri, Serikali inapendekeza kufuta Ada na Tozo ambazo zinatozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) kama ifuatavyo:

i Kufuta Ada ya Kiingilio (entry fee) kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyengine ya TZS 1000 kwa siku, kwa gari binafsi na za kusafirisha abiria.

ii Kufuta Ada ya Njia ya TZS 3,000 kwa siku,

iii Kufuta Ada ya Beji ya udereva na Utingo kwa gari za biashara ya TZS 50,000 kwa kila mmoja kwa mwaka na

iv Kufuta Ada ya Ruhusa ya Njia (Route) kwa gari za abiria ya TZS 50,000 kwa mwaka.

Kwa hatua hizi, Gari za abiria (public transport) zitalipa Ada ya Huduma ya Usafi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) ya TZS 50,000 kwa mwaka wakati wanaomba Ruhusa ya Njia kutoka Idara ya Usafiri na Leseni.

v Kufuta Ada ya asilimia 2 ya mauzo ya tiketi kwa kila "trip" inayotozwa kwa wenye vyombo vya usafirishaji wa abiria na mizigo Baharini.

121. Mheshimiwa Spika; Katika Sekta ya Nishati (Vituo vya Mafuta), Serikali inapendekeza hatua zifuatazo:

i Kufuta Ada ya Usafi kwa Vituo vya Mafuta ya TZS 50,000 hadi 100,000 kwa mwezi (sawa na TZS 600,000 hadi 1,200,000 kwa mwaka) inayotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuweka kiwango kimoja cha TZS 600,000 kwa mwaka ambacho kitalipwa na wenye Vituo wakati wanaomba leseni.

ii Kuandaa muongozo wa pamoja utakaowezesha wenye Vituo vya mafuta kulipa Ada na Tozo za Wizara ya Biashara na Viwanda na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) wakati wanaomba Kibali cha kuendesha Biashara hizo.

122. Mheshimiwa Spika; Katika Sekta ya Kilimo na Uvuvi, Serikali inapendekeza hatua zifuatazo:

i Kufuta Vibali vya Usafirishaji wa Mazao, ambavyo hukusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) kupitia kwa Masheha. Vibali hivyo vitatolewa bila ya malipo ili kuongeza udhibiti zaidi kwa mazao hayo.

ii Kufuta Ada na Tozo zote vinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) kwa wafanya biashara wa wanaoanika dagaa. Hivyo, Kibali cha Biashara ya Dagaa cha TZS 2,000 kwa siku na Ada ya Uratibu wa mazao ya Bahari ya TZS 10,000 hadi 20,000 kwa mwezi, vinafutwa.

iii Kufuta Ada na Tozo zote zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) katika Zao la Karafuu. Hivyo, Ada ya Kusafirisha Karafuu ya TZS 3,000 hadi 5,000 kwa gunia na Ada ya ukodishaji wa mikarafuu ya asilimia 5.

iv Kufuta Ada na Tozo zote zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) katika Zao la Mwani. Hivyo, Ada ya Kusafirisha Mwani ya TZS 2,000 kwa tani; Ada ya Uratibu wa mazao ya Bahari ya TZS 10,000 hadi 20,000 kwa mwezi na Tozo ya Usafirishaji wa Mazao ya Baharini ya TZS 3,000 – 10,000 kwa gunia.

X. SURA YA BAJETI

123. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2020/2021, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya TZS 1,579.2 bilioni ikihusisha:

a. Mapato ya Ndani ni TZS 1,050 bilioni;

b. Ruzuku na Mikopo kutoka nje ni TZS 423.2 bilioni.
c. Marejesho ya Mkopo kutoka Benki ya Exim ya China TZS 61 bilioni; na
d. Mikopo ya Ndani ni TZS 45.0 bilioni.

124. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Matumizi, kiasi hicho cha jumla ya TZS 1,579.2 bilioni kinatarajiwa kutumika kama ifuatavyo:

i. Matumizi ya Kazi za Kawaida TZS 969.3 bilioni, ikijumuisha Mishahara ya Mafungu TZS 316.8 bilioni na Mishahara ya Ruzuku TZS 123.8 bilioni, Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida TZS 182.6 bilioni, Ruzuku OC ya Mafungu 170.1 bilioni na matumizi ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali TZS 237.9 bilioni;
ii. kwa upande wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo jumla ya TZS 609.9 bilioni, ikihusisha TZS 197.3 bilioni fedha za Serikali na TZS 412.6 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zikiwemo (Mikopo TZS 340.5 bilioni na Ruzuku TZS 82.7 bilioni).

125. Mheshimiwa Spika, Kwa sura hii ya Bajeti, kunajitokeza taswira ifuatayo:

i. Mapato ya ndani ya TZS 1,050 bilioni sawa na asilimia 66.5 ya makadirio ya bajeti hivyo

yatakidhi kugharamia matumizi yetu yote ya kazi za kawaida ya jumla ya TZS 969.3 bilioni sawa na asilimia 61.4 ya makadirio ya bajeti.

ii. Mpango wa Maendeleo, umekadiriwa kutumia asilimia 38.6 ya makadirio ya bajeti yote zikiwemo TZS 197.3 bilioni sawa na asilimia 12.5 ya makadirio yote na TZS 412.6 bilioni sawa na asilimia 26 ya makadirio ya bajeti kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, kupitia vyanzo vifuatavyo vya fedha:

a) Mapato ya Ndani ya TZS 152.4 bilioni (ikihusisha mapato ya Mfuko wa Miundombinu TZS 44.2 bilioni);
b) Mikopo kutoka nje TZS 340.5 bilioni;
c) Ruzuku kutoka nje TZS 72.1 bilioni, na
d) Mikopo ya Ndani ni TZS 45.0 bilioni.

126. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kiwango cha Ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ya TZS 82.6 bilioni na makadirio ya matumizi ya TZS 1,579.2 bilioni, kiwango cha utegemezi wa Bajeti kinatarajiwa kushuka zaidi na kufikia asilimia 5.2 kwa mwaka 2020/2021 kutoka asilimia 6.7 iliyoripotiwa mwaka uliopita. Mfumo kamili wa Bajeti kwa mwaka 2020/2021-2022/2023 ni kama unavyonekana katika jadweli hapa chini.

MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA 2020/2021-2022/2023						
				Tarakimu kwa TZS Bilioni		
Maelezo	**Makisio 2019/20**	**Matarajio 2019/20**	**Makisio 2020/21**	**Makisio 2021/22**	**Makisio 2022/23**	**% ya Bajeti**
MAPATO						
Marejesho ya Mkopo	-		61.0			
Mapato ya Ndani	976.5	835.3	1,050.0	1,154.3	1,297.5	85.5
Mikopo na Ruzuku kutoka Nje (ODA)	402.9	283.5	423.2	340.1	441.7	70.4
Mkopo wa Ndani	40.0	40.0	45.0	40.0	40.0	100.0
Jumla ya Mapato	**1,419.4**	**1,158.8**	**1,579.2**	**1,534.4**	**1,779.2**	81.6
MATUMIZI						
Matumizi ya Kawaida	***842.4***	***740.0***	***969.3***	***966.8***	***1,090.7***	***87.8***
Mshahara Mafungu	301.5	248.3	316.8	332.6	393.4	82.4
OC Mafungu SMZ	168.6	148.8	172.0	169.2	253.7	88.3
OC kutoka kwa Washirika wa Maendeleo	-		6.8	4.0	2.4	
Mfuko Mkuu wa Serikali	158.2	152.3	237.9	200.5	173.8	96.3
Mshahara Ruzuku	108.1	115.5	123.8	130.0	122.6	106.8
OC Ruzuku	97.7	72.3	108.2	119.3	140.6	74.0
OC Kutoka Mfuko wa Pamoja BF	8.3	2.8	3.8	11.2	4.2	33.7
Matumizi ya Maendeleo	***577.0***	***418.8***	***609.9***	***567.6***	***688.6***	***72.6***
Fedha za SMZ	182.4	135.3	197.3	233.3	250.2	74.2
Mikopo na Ruzuku kutoka Nje (ODA)	394.6	283.5	412.6	334.4	438.3	71.8
Jumla ya Matumizi	**1,419.4**	**1,158.8**	**1,579.2**	**1,534.4**	**1,779.2**	**81.6**

Chanzo: **Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar**

XI. MAENEO MAALUM

127. Mheshimiwa Spika, kwa miaka kadhaa sasa zao la mwani limejitokeza kuwa na umuhimu maalum kama zao la biashara, linalotoa ajira kwa wananchi wengi wa vijijini hasa akina mama na hivyo kusaidia sana katika kupunguza umaskini. Kama ilivyo kwa karafuu, utaratibu wa sasa kwa zao la mwani ni kuzalishwa, kuanikwa na kusafirishwa ukiwa ghafi, bila ya usarifu wa kuuongezea thamani. Kwa sababu hii, kumekuwa na malalamiko ya bei wanayolipwa wakulima kuwa ndogo. Kwa upande mwengine, kuna pia malalamiko ya wanunuzi juu ya kodi na ada mbalimbali zinazotozwa katika zao hilo.

128. Mheshimiwa Spika, Serikali imefanyia kazi hali hii na inaelekea kwenye kuyapatia ufumbuzi. Kufuatia ziara ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nchini Indonesia mapema mwaka 2019, Serikali imefanikiwa kupata wataalamu wa kuangalia kwa kina ukulima wa mwani wa Zanzibar na kubainisha mambo kadhaa yanayohitaji kurekebishwa ikiwemo katika ukulima wake, ukaushaji na utambuzi sahihi wa aina yake. Mambo haya yamesaidia sana katika kuimarisha bei ya mwani hapa nchini na hivyo kusaidia kipato cha wakulima wake.

129. Mheshimiwa Spika, nina furaha kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa Serikali imeamua kujenga kiwanda

cha kusarifu mwani katika eneo la Chamanangwe, kisiwani Pemba. Mtaji wa mradi huo unaotarajiwa kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha unatokana na michango ya mashirika na taasisi za Serikali ambazo ndio zitakuwa wamiliki wakuu wa hisa. Ni imani yetu kwua uamuzi huu utasaidia zaidi katika kuliimarisha zao hilo kwani utatoa soko la uhakika na lenye bei nzuri kwa wakulima.

130. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kidemokrasia, kila baada ya miaka mitano nchi yetu inapitia kitendo maalum cha kuchagua uongozi wa kusimamia maendeleo yetu katika miaka mitano inayofuata. Kwa mujibu wa Katiba yetu na Sheria, kazi hiyo kufanyika kupitia Uchaguzi Mkuu ambao matokeo yake ni kutupatia Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Wawakilishi wetu katika Baraza hili tukufu, katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na Madiwani wa kutuwakilisha katika Serikali za Mitaa.

131. Mheshimiwa Spika, panapo uhai, mwishoni mwa mwaka huu tunatimiza tena miaka mitano ya kipindi cha pili cha awamu ya saba ya SMZ na hivyo tunataraji kufanya Uchaguzi Mkuu mwengine, utaoshirikisha ushindani wa vyama vingi vya siasa. Kwa bahati mbaya, hapa kwetu kuna changamoto ya kutoaminiana kwa vyama vya siasa na kupelekea matokeo ya uchaguzi kulalamikiwa. Imetokea hivo

kwa chaguzi zote zilizowahi kufanyika Zanzibar na kushindaniwa na vyama vingi vya siasa, kabla na baada ya Mapinduzi. Hatujawahi kufanya uchaguzi Zanzibar tukiwa na vyama vingi na usilalamikiwe.

132. Mheshimiwa Spika, sote tunapaswa kuitafakari hali hii; lazima tuipatie suluhisho la kudumu. Kwa kuanzia, tujenge utamaduni wa kuaminiana. Kidhati kabisa kila Chama cha siasa kitachoshiriki uchaguzi mkuu ujao kiwaelimishe wanachama wake kujiepusha na vitendo vyote vitavyopelekea kuendeleza hali tete ya kisiasa hapa Zanzibar. Wote tujizatiti kuhakikisha kuwa tunaepuka kutumiwa na mashirika na mataifa mengine kutuletea mtafaruku na kumomonyoka umoja na udugu wetu sisi ni wamoja na umoja wetu ni wa asili.

133. Mheshimiwa Spika, Sisi tumedhamiria kugharamia wenyewe na kuusimamia vyema Uchaguzi Mkuu wa mara hii baada ya changamoto kubwa zilizojitokeza uchaguzi wa mwaka 2015 hadi kupelekea kufutwa kwake, ambazo tunaelewa kuwa zilikuwa na mkono wa wasiotakia mema nchi yetu. Silalamikii ushindani wa siasa za vyama vingi, la hasha. Vyama vingi vimeruhusiwa na Katiba ya nchi na vinapaswa kushindana. Ninanchosisitiza ni kuwa kuna haja kwa vyama kushindana kistaarabu zaidi, kwa kuaminiana zaidi na kwa kutanguliza mbele umoja wetu, amani yetu na utulivu wetu. Wakati umefika kwa Zanzibar

kufungua ukurasa mpya wa kisiasa; uchaguzi mkuu mwaka huu ni fursa hiyo.

134. Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, ni wajibu wangu kukitakia mema na ushindi mkubwa zaidi katika uchaguzi huo, Chama changu, **Chama Cha Mapinduzi!** Nna amini wananchi walio wengi wataendelea kukiunga mkono, kuzikubali Sera zake bora na kukipa kura nyingi katika uchaguzi huo ili kiendelee kuwatumikia katika kuiongoza nchi yetu. Uchumi na ustawi utazidi kuimarika tu penye amani na utulivu, mambo ambayo CCM imejidhihirisha kuwa inayalinda na kuyadumisha.

XII. SHUKURANI

135. Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza Hotuba yangu hii naomba uniruhusu nitoe shukrani maalum. Kwanza, kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa uongozi wake thabit, dhamira yake ya dhati ya kuwaletea Wazanzibari wote maendeleo ya haraka na maelekezo yake katika maandalizi ya Bajeti hii. Tuliobahatika kuwa karibu na Dkt. Shein hasa katika kipindi hiki cha kukabiliana na janga la maradhi ya corona, tumeshuhudia kwa mara nyengine tena uongozi imara, usioyumba na wenye hekima kubwa sana kutoka kwake. Kwa hakika tumejifunza mengi katika kujipambanua katika kufikiri, kujali zaidi

wananchi tunaowaongoza na kufanya uamuzi kwa kushauriana na viongozi wengine na wataalamu bila ya kukurupuka na kuiga tu ya wengine. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

136. Mheshimiwa Spika, bila ya shaka, kama nilivyosema awali, mshauri mkuu wa Mheshimiwa Rais ni Makamu wake wa Pili, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi ambae pia ametuongoza kwa umahiri mkubwa, upande wa Serikali, katika shughuli za Baraza letu hili. Namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Seif.

137. Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza letu hili ambalo ni nguzo adhimu kwa mustakabali wa nchi yetu, Naibu wako Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar na Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma kwa kazi kubwa ya kuliendesha kwa umahiri mkubwa Baraza hili kwa miaka mitano hii inayomalizika na katika kikao hiki cha bajeti. Mmetuvusha salama na kwa mashirikiano na maelewano makubwa na mihimili mingine ya Dola, Serikali na Mahkama. Nakushukuru na kukupongeza sana.

138. Mheshimiwa Spika, nazishukuru pia Kamati zote za Kudumu za Baraza hili kwa kazi kubwa ilizofanya muda wote kulisaidia Baraza katika kufuatilia

utendaji was keta zake na Serikali kwa ujumla. Natoa shukrani makhsusi kwa Kamati nilizofanyakazi nazo kwa karibu zaidi ikiwemo ya Bajeti, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Mohammed Said Mohammed (Dimwa). Kamati nyengine ni ya Fedha, Biashara na Kilimo iliyoongozwa vyema na mzoefu Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Mashirika (PAC) chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa na Kamati ya Kanuni iliyoongozwa na Mheshimiwa Rashid Makame Shamsi. Nawashukuru wao na wajumbe wote kwa kazi yao nzuri.

139. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Watendaji, nashukuru sana mchango mkubwa na wa mfano wa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee. Aidha, mashirikiano makubwa tumeyapata kutoka Wizara zote hivyo kwa fursa hii, nashukuru sana utendaji wa Makatibu Wakuu na watendaji wote.

140. Mheshimiwa Spika, pamoja na michango ya watu mbalimbali, bado kazi kubwa imefanyika ndani ya Wizara yangu na Tume ya Mipango. Namshukuru na kumpongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Bwana Khamis Mussa Omar, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango – Bwana Mwita Mgeni Mwita. Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango – Bwana Khatib Mwadini Khatib, Mhasibu

Mkuu wa Serikali - Bi Mwanahija Almas Ali, Naibu Mhasibu Mkuu wa Serikali - Bwana Ame Burhani Shadhil, Kamishna wa Bajeti Dkt. Suleiman Simai Msaraka, Kamishna wa Fedha za Nje Bi Bihindi Nassor Khatib na Mkurugenzi wa Sera za Kodi na Fedha Bwana Khamis Shibu Mwalim. Kupitia kwao, nawashukuru watendaji wote wa Wizara, Tume ya Mipango na Taasisi zilizo chini ya Wizara hususan Mamlaka ya Mapato (TRA) na Bodi ya Mapato (ZRB).

141. Mheshimiwa Spika, siwezi kumaliza hotuba yangu hii bila ya kutoa shukran maalum; kwa niaba ya Serikali, wananchi na mimi mwenyewe binafsi. Kuna wakati tunasahau kuwa katika utulivu wetu, katika amani yetu na katika uzima wetu kuna watu ambao wanajitolea maisha yao. Tusipuuze kazi kubwa inayofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Sisi sote tunapata usingizi mnono kwa sababu wenzetu wao hawalali ili kulinda usalama wetu. Nawashukuru kwa dhati sana Makamanda, askari na wapiginaji wote wa vyombo vya ulinzi na usalama.

142. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru sana watu wote waliokuwa katika mstari wa mbele katika kupambana na maradhi ya COVID-19. Wenzetu hawa wamefanya kazi kubwa kulinda maisha yetu sote dhidi ya janga la corona. Tunawashukuru, tunawathamini na tunajivunia sana uzalendo na ujasiri wao wa kupigiwa mfano.

Nilikusudia niwataje wote kwa majina ili waingie katika kumbukumbu zetu hapa Barazani. Hata hivyo, kwa idadi yao ya watu 509, ni wengi hivyo naomba wakubali na wapokee shukurani hizi kwa makundi yao kama ifuatavyo:

i. Uratibu na Ufuatiliaji (RRT) Unguja – watu 73;
ii. Uratibu na Ufuatiliaji Pemba - wattu 38;
iii. Mawasiliano na elimu kwa Umma (RCCE) – watu 30;
iv. Kituo cha matibabu Kidimni – watu 64;
v. Kituo cha matibabu JKU – watu 61;
vi. Kituo cha Matibabu Kidongochekundu – watu 51;
vii. Vituo vya Matibabu Pemba – watu 53;
viii. Timu za Ufuatiliaji kiwilaya Unguja (DST)– watu 56;
ix. Timu za Ufuatiliaji Kiwilaya Pemba – watu 48; na
x. Timu za maziko – watu 35.

AHSANTENI SANA MADAKTARI, WAUGUZI NA WATENDAJI WOTE WA MSTARI WA MBELE KWA KAZI KUBWA NA NZURI!

Nawashukuru pia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wote wa Unguja na Pemba kwa kazi yao nzuri ya kuelimisha jamii yetu na kusimamia kidete utekelezaji wa maagizo ya Serikali na ushauri wa wataalamu wetu wa afya.

143. Mheshimiwa Spika, nashukuru pia nchi rafiki na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa yanayoendelea kushirikiana nasi katika maendeleo yetu ikiwemo nchi za Bahrain, Canada, Cuba, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Jamhuri ya watu wa China, Hispania, Indonesia, Israel, Itali, Korea ya Kusini, Kuwait, Malaysia, Marekani, Misri, Norway, Oman, Saudi Arabia, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Uturuki.

144. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mashirika, tunashukuru na kutahmini msaada na mashirikiano ya: AfDB, , BADEA, , EU, EXIM Bank ya China, EXIM Bank ya Korea, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD, ILO, IMF, IPEC, JICA, NORAD, OFID, ORIO-Netherlands, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, UNAIDS, UN, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-HABITAT, UNICEF, UNIDO, USAID, WB, WHO, WFP na WSPA, AUCLAND UNIVERSITY, OPEC, URT, KOICA, NORWAY,GPE, UN Women, China, India World Diebetic Foundation, BASKET FUND, GN , IITA, NORAD, MILELE, Partnership for Child Development.

I. HITIMISHO:

145. Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Makadirio ya Mapato ya Serikali ya kukusanya jumla ya Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia tano Sabini na Tisa na Milioni Mia Mbili

(TZS 1,579.2) kwa mwaka wa fedha, 2020/2021. Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani ni TZS 1,050 bilioni na na TZS 45.0 bilioni ni mikopo ya ndani. Aidha, Ruzuku na Mikopo kutoka Nje ni TZS 419.4 bilioni, TZS 3.8 bilioni ni Ruzuku kwa Mfuko wa Pamoja wa wafadhili (Basket Fund) na TZS 61 bilioni ni Marejesho ya matumizi ya SMZ kupitia mkopo kutoka Benki ya Exim ya China.

146. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, nina heshima ya kuliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia tano Sabini na Tisa na Milioni Mia Mbili (TZS 1,579.2 bilioni) kwa mwaka huo wa fedha wa 2020/2021. Kati ya matumizi hayo, TZS 969.3 bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS 609.9 bilioni kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

147. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa (MBM),
WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO,
ZANZIBAR.
15 JUNI 2020.

PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA MFUKO WA MIUNDOMBINU (INFRASTRUCTURE FUND) TZS "000"

KIFUNGU	JINA LA PROGRAMU/MRADI	MAKISIO KWA MWAKA 2019/20 SMZ	MAKISIO KWA MWAKA 2020/21 SMZ
C01	**OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS**		
	i) Ujenzi wa Nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais	350,000	
	JUMLA YA FUNGU	**350,000**	**-**
F01	**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**		
	Programu ya Upatikanaji Rasilimali Fedha	300,000	
	JUMLA YA FUNGU	**300,000**	**0**
L01	**WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI**		
	Programu ya Kuimarisha Uvuvi		
	i) Uimarishaji Uvuvi wa Bahari Kuu	1,400,000	2,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**1,400,000**	**2,000,000**
R01	**WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA**		
	i) Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar	2,000,000	3,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**2,000,000**	**3,000,000**
K01	**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**		
	i) Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali - Awamu ya Pili	1,000,000	
	JUMLA YA FUNGU	**1,000,000**	**0**
H01	**WIZARA YA AFYA**		
	Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya		
	i) Ujenzi wa Hospital ya Rufaa Binguni (Awamu ya Kwanza)	6,000,000	6,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**6,000,000**	**6,000,000**
N01	**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, MAJI NA NISHATI**		
	i) Kuendeleza Visima vya Ras el Khaimah	3,000,000	2,000,000
	ii) Usambazaji Umeme Vijijini	650,000	500,000
	JUMLA YA FUNGU	**3,650,000**	**2,500,000**
P01	**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI**		
	Programu ya Ujenzi wa Barabara		
	i) Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake-Wete	1,000,000	
	ii) Ujenzi wa Barabara za Ole- Kengeja	5,600,000	
	iii) Ujenzi wa Daraja la Uzi-Ng'ambwa		5,000,000
	Mradi		
	i) Ununuzi wa Land Craft	1,900,000	2,400,000
	JUMLA YA FUNGU	**8,500,000**	**7,400,000**
G07	**MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI**		
	Ujenzi wa Ofisi ya ZAECA	800,000	1,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**800,000**	**1,000,000**
J02	**KAMISHENI YA UTALII**		
	Kuimarisha Utalii kwa Wote	1,500,000	2,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**1,500,000**	**2,000,000**
S01	**WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**		
	Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya	2,000,000	2,500,000
	JUMLA YA FUNGU	**2,000,000**	**2,500,000**
D01	**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ**		
	i) Uwekaji wa Kamera na Vifaa vya Ulinzi	7,000,000	8,000,000
	ii) Ujenzi wa Kiwanda cha Ushoni (ZQTL)	3,600,000	1,400,000
	JUMLA YA FUNGU	**10,600,000**	**9,400,000**

D02	**JESHI LA KUJENGA UCHUMI**		
	i) Ujenzi wa Skuli ya Sekondari na Ufundi - Mtoni		2,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**0**	**2,000,000**
D04	**KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)**		
	i) Kuimarisha Huduma za Uzamiaji na Uokozi	2,900,000	4,800,000
	JUMLA YA FUNGU	**2,900,000**	**4,800,000**
D05	**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI**		
	i) Ununuzi wa Vifaa vya Zimamoto		1,600,000
	JUMLA YA FUNGU	**0**	**1,600,000**
	JUMLA KUBWA	**41,000,000**	**44,200,000**